**6 JUNI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 6 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Sasa nimwite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika nchi yetu kumekuwa na sheria, sera, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali kwa watumishi wa Serikali na taasisi zake kuzingatia muda wa kuingia kazini na muda wa kutoka kazini, lakini kumekuwa na changamoto kwenye baadhi ya watumishi wa kada moja kutofautiana muda wa kutoka kazini, kwa mfano, walimu wa shule za msingi mijini wanatoka kazini saa 8.30 mchana lakini wale wa vijijini wanatoka mpaka saa 10.30 alasiri.

Je, Serikali haioni haja ya kupitia upya utaratibu huu ili kuweka sawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha leo kuwa na uhai, uzima na hatimaye leo asubuhi hii tunaanza programu zetu kwa kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kisangi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inayo sheria ya kazi ambayo inaainisha pia muda wa kuingia kazini na muda wa kutoka kazini na kwa mujibu wa sheria zetu muda wa kazi Kiserikali ni saa zisizopungua nane, kuanzia saa 1.30 asubuhi mpaka saa 9.30 alasiri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia utofauti wa muda wa kutoka kwa walimu wa shule za msingi wa mijini na vijijini, kwa bahati nzuri na mimi pia ni mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachopelekea utofauti wa muda wa kutoka ni mazingira ya maeneo hayo ya miji na vijijini. Maeneo ya mijini mara nyingi ofisi za elimu na kwa kupata kibali kutoka TAMISEMI wanafunzi wakiingia asubuhi na walimu wakiingia asubuhi mchana hawapati muda wa kwenda kupumzika na kwa hiyo, wanaunganisha mpaka saa 8.30 mchana, lakini vijijini muda wa mchana wanapata nafasi ya kurudi nyumbani kwenda kula.

Kwa hiyo, ule muda wa kula ndio unaokuja kulipiwa pale mbele na kufanya muda wa kutoka uonekane kuwa ni mrefu zaidi, lakini saa za kazi ni zile zile. Kwa hiyo, huu ni mpango kazi uliowekwa kulingana na mazingira yaliyopo ya mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa nini huku mijini wanaamua kuunganisha moja kwa moja? Kwanza kuna shida ya usafiri, huwezi kuruhusu mwanafunzi mchana arudi nyumbani, aende shule utaona mazingira kama Jiji la Dar es Salaam mazingira yale mwanafunzi kutoka nyumbani kwenda shuleni peke yake shida, ukimruhusu mchana saa moja arudi nyumbani, halafu arudi tena saa saba bado ni shida vilevile, kwa hiyo wanaamua kuunganisha moja kwa moja na ndio sababu wanaonekana wanaingia saa 1.30 asubuhi na kutoka saa 8.30 mchana.

Mheshimiwa Spika, lakini vijijini kwa sababu hakuna tatizo la usafiri na shule za msingi ziko vijijini, kwa hiyo, ni kiasi cha kutembea kwenda nyumbani anapumzika, anakula, anarudi shule na ule muda alioutumia kwa kula unasogezwa mbele na kwa hiyo, muda wa kuondoka shuleni unaongezeka na kwa hiyo, hata walimu nao wanatoka muda huo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni mpango kazi ambao pia umeridhiwa na TAMISEMI, kwa hiyo tuchukue hiyo tuipeleke TAMISEMI waone kama kuna umuhimu wa hata vijijini kuunganisha muda bila kuruhusu wanafunzi wetu kupata chakula, hiyo pia inaweza kuamriwa na Wizara kulingana na mahitaji na mazingira yalivyo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa ya kujenga madarasa kwenye shule zote za msingi na sekondari na wakati mwingine imejenga shule iliyokamilika, kutokana na kufanya kazi hii tumeongeza wanafunzi wengi na

kutokana na kuongezeka kwa wanafunzi tumeongeza upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Spika, ziko halmashauri na majiji ambayo yanakusanya fedha nyingi, lakini nao wanasubiri mgao wa ajira hususan kama ya walimu waweze kupata sawa na halmashauri zingine ambazo hazina mapato.

Je, Serikali haioni kama ni busara na ni vyema kwamba halmashauri na majiji ambayo yana uwezo wa kuajiri walimu waweze kuajiri ili inavyokuja ule mgao wa kitaifa hawa wengine ambao hawana tuwe tumewapunguzia mzigo huo na kufanya hivyo ni kwamba maeneo yale tayari tutakuwa tumeondoa tatizo la walimu? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nollo, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imesimamia mifumo ya ajira na ajira zote za kudumu ziko chini ya Serikali Kuu ikiwemo na sekta ya elimu kwa walimu. Nikiri kwamba tunao upungufu wa walimu kwenye shule zetu za msingi hata sekondari na upungufu huu unatokana na vipindi vya ajira, lakini hapa katikati kabla ya ajira kunakuwa na vifo kunakuwa na kustaafu lakini pia hata mpango usiokuwa mzuri wa kwenye halmashauri zenyewe kwa sababu walimu wengi wanaonekana wanajaa sana mijini kuliko vijijini, nitalisema baadae.

Mheshimiwa Spika, kwa nini ajira zote zimepelekwa Serikali Kuu? Lengo ni kuwa na mfumo mmoja wa kuajiri na kupata kanzidata yaani takwimu ya idadi ya waliopo kazini wanaoajiriwa, lakini pia kuweza kusambaza kwa usawa kwenye halmashauri zote ili kusiwe na halmashauri moja kuwa na mlundikano mkubwa kwa sababu tu wana uwezo wa wao kuajiri. Kwa hiyo, Serikali Kuu inasimamia kusambaza walimu nchini kote kulingana na mahitaji, kulingana na fani walizosomea, kwa mfano, masomo ya sayansi

na masomo ya sanaa hiyo. Kwa hiyo, mahitaji yanakwenda nchini kote.

Mheshimiwa Spika, tunajua ziko halmashauri zenye uwezo, lakini kuna halmashauri ambazo hazina uwezo. Tukiruhusu halmashauri zenye uwezo ziajiri kuna hatari ya halmashauri ambazo zinapata pato chini ya uwezo wake hakutakuwa na walimu hakutakuwa na wafanyakazi na kwa hiyo, hakutakuwa na usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali hatuwezi kuruhusu hili na ndio sababu ajira zote tumeweka za Serikali Kuu yenyewe inaajiri walimu 4,000 tunawagawa nchi nzima kulingana na idadi, uwiano wa masomo kwa maana ya fani, lakini na mahitaji ya hizo halmashauri. Tutaendelea kufanya hivi inatusaidia pia Serikali katika kulipa stahiki zao pamoja na mafao yao ya mwisho wa kustaafu, lakini pia inatusaidia kuwa na takwimu.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, sasa nitoe agizo kwa Maafisa Elimu na Wakurugenzi wa Halmashauri kufanya mapitio ya ikama zao. Hapa ndipo tatizo lilipo kwamba halmashauri inaruhusu eneo fulani kuwa na walimu wengi halafu kule vijijini hakuna walimu na kusababisha kuwa na upungufu mkubwa wa walimu, kumbe kama wangekuwa wamewasambaza vizuri ingekuwa na walimu wanaotosha kwenye fani zao. Kwa hiyo, wapitie ikama yao ili wajaribu kuona mlundikano wa walimu kwenye maeneo ya miji na barabarani ili wawapeleke pia na vijijini kuwe na utoshelevu halafu ile kanzidata isaidie pia katika kufanya kila shule kuwa na idadi nzuri ya walimu, hizi ndio sababu ambazo zinapelekea Serikali Kuu kuajiri *centrally*, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu.

**MHE. EMMANUEL E. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi hii ya kuuliza swali kwa Waziri kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapa nchini Serikali imekuwa ikitoa 10% ya mikopo kwa walemavu, wanawake, lakini pia vijana ambao wako chini ya miaka 35, lakini kuna kundi hili ambalo linazidi miaka 35 ambalo ndio mhimili mkubwa wa familia na ndio walipa ada wakubwa kwa watoto na ndio wanaotibisha familia, lakini pia ndio kundi ambalo linalinda uchumi wa familia.

Sasa ni nini mkakati mkubwa wa Serikali wa kuweza kulikumbuka kundi hili katika masuala ya mikopo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa amelitamka kundi hili, kundi hili, kundi hili hajalitaja kundi hilo ni kundi gani au labda sikusikia vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, anamaanisha kundi ambalo wamevuka umri wa ujana, siyo wanawake na wala hawana ulemavu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imetenga fungu maalum la mapato ya ndani katika kila halmashauri kutoa fursa za kuendeleza ujasiriamali kwa kutoa mikopo midogo midogo na ya kati kwa makundi ya wanawake 4%, walemavu 2% na vijana 4%. Sasa kundi hili la zaidi ya miaka 35 sio kwamba tumelisahau bali tunazo fursa nyingine za kupata mitaji kupitia mifuko mbalimbali, lakini pia kwenda kwenye taasisi za fedha kama vile mabenki na ile mifuko ambayo imepata vibali maalumu vya kukopesha.

Mheshimiwa Spika, haya makundi tunayoyazungumza kutokana na tathmini za ndani za Serikali ziko changamoto zinazokabili makundi haya ya vijana, lakini pia walemavu na wanawake. Mpango wetu ni kuhakikisha kwamba makundi haya nayo yanakuwa na eneo ambalo wanaweza kwenda kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kuwapa faraja Watanzania kwamba Serikali imeendelea kuzungumza na benki kwa maana ya taasisi za fedha kufungua madirisha ya kutoa mikopo ya viwango mbalimbali kulingana na mahitaji ya mteja mwenyewe na huku ndiko ambako pia tunaruhusu hili kundi la watu kutoka miaka 35 na kuendelea ili kuweza kupata mikopo na kwa hiyo, kadiri Serikali itakapokuwa na uwezo itaendelea kufungua milango na kuanzisha mifuko mingine ili kutoa fursa kwa makundi mengi zaidi kupata mikopo kama mitaji kwa ajili ya shughuli zao za ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kupata nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, michezo ya kubashiri imekuwa ikichangia Pato la Taifa, lakini mapato ya michezo hii yamekuwa hayanufaishi moja kwa moja sekta ya michezo kutokana na michezo hii kusimamiwa na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, Serikali haioni haja ya kuihamisha michezo hii kutoka kwenye Wizara ya Fedha kuipeleka kwenye Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba tunayo michezo ya kubahatisha na kubashiri michezo ambayo inaratibiwa na Bodi ya Bahati Nasibu na makampuni haya yanayoendesha ubashiri wa michezo wanalipa kodi na kwa mujibu wa sheria zetu nchini kodi

zote huwa zinapewa mamlaka inayokusanya kodi ambayo huwa ni *TRA*.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge anataka kusema kwa nini kibali hiki kisipewe Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kuweza kuendeleza michezo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hii Bodi ya Michezo ya Kubahatisha iko Wizara ya Fedha na anayekusanya mapato ni *TRA* kama ambavyo kodi zingine zinavyokusanywa na *TRA*, lakini baada ya kukusanya fedha hii Baraza la Michezo lililoko ndani ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo linapata mgao wa 5% ya makusanyo ya fedha kutoka kwenye michezo hii ya kubahatisha na kwa hiyo suala la uendelezaji wa michezo linabaki pale pale, kwa sababu hiyo 5% ndiyo inayotakiwa kukusanywa na hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lengo la kuipa *TRA* kukusanya mapato ni katika kudhibiti mianya ya fedha katika kuweka uelewa wa taasisi husika ya ukusanyaji kodi ambao pia ni *TRA* na mamlaka ambayo imepewa na kwa hiyo sasa tuna uhakika kila ikikusanya tukishapata takwimu 5% tunapeleka kwenye mfuko wa kuendeleza michezo ulioko chini ya Baraza la Michezo kwa ajili ya shughuli za michezo na ndiyo utaratibu ambao kwa sasa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, pia kama wadau wa michezo wataona kuna haja ya kuishauri Serikali, sisi tunapokea ushauri na kupitia vikao vyetu tutabadilisha kanuni na sheria zetu ili tuelekeze huko kama umuhimu upo kwa ajili ya kuendeleza michezo kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Wakuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na nchi yetu uchumi kuboreka na kuendelea kukua na hali ya amani iliyopo katika Taifa letu, kumekuwa na ongezeko kubwa sana la wafanyabiashara wa ndani ya nchi, lakini vilevile wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nje kitendo ambacho kimekuwa kikipanua na kuendelea kuweka wigo mpana zaidi kwenye ufanyaji wa biashara.

Mheshimiwa Spika, lakini kumekuwa kuna tatizo kwamba baadhi ya wafanyabiashara na wawekezaji ambao wanakuja kufanya biashara hapa Tanzania wamekuwa wakifungua biashara au wakifungua viwanda, lakini wamekuwa wanakwenda kwenye ngazi ya chini kabisa kule vijijini kitu ambacho kinasababisha wale Watanzania ambao ni wafanyabiashara au watanzania wananchi wa kawaida kushindwa kufaidika na biashara hizi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kujua, je ni lini Serikali italeta sera nzuri ili kuweza kumnufaisha Mtanzania huyu walau baadhi ya wafanyabiashara wafikie kwenye *level* fulani waishie huko kwenye uzalishaji na huku kwenye usambazaji na kufungua maduka mengine mpaka ngazi za chini kazi hizi zifanywe na Watanzania kama ilivyo kwenye baadhi ya nchi za wenzetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nitambue mchango wa wafanyabiashara wadogo ambao wananchangia sana kwenye pato letu la Taifa kutokana na shughuli zao za kibiashara, wanalipa kodi na tunaendelea kutunisha mfuko wetu. Pia nchi yetu inayo sera ya mahusiano ya kidiplomasia na nchi marafiki ambao pia wamefungua milango kuingia nchini kufanya shughuli mbalimbali ikiwemo biashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu pia inazo sheria na kanuni ambazo zinaongoza wageni hawa kufanya shughuli mbalimbali hapa nchini ikiwemo biashara, lakini kwa vibali maalumu ambavyo pia vinazingatia aina ya biashara ili kuruhusu Watanzania kufanya biashara nyingi huku ndani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwingiliano wa wengine kuacha biashara ya ngazi yao kulingana na vibali vyao na kufanya biashara ambazo Watanzania wangeweza kufanya, Serikali tumeimarisha ufuatiliaji wa vibali hivi ambavyo tumevitoa kwa hawa wageni ambao wanafanya biashara ili kuzuia kuingia kufanya biashara ambazo ni fursa kwa Watanzania ili waweze kujipatia mapato yao.

Kwa hiyo, taasisi ambayo inatoa vibali vya kazi inazingatia sana vibali wanavyovitoa ili kuzuia mianya ya wageni kuja kufanya biashara za wananchi wa Tanzania ikiwemo biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, hili ndilo ambalo Serikali yetu imeweka mazingira ya wafanyabiashara wadogo kufanya biashara zao kwenye maeneo maalumu kama vile hapa Dodoma eneo la *Machinga Complex,* lakini maeneo mengine yote tulitoa kibali cha halmashauri kuandaa maeneo ya wafanyabiashara wadogo ili isaidie hata ukaguzi na ufuatiliaji tunaoufanya wa kukuta wageni ambao hawakupata vibali vya kufanya biashara hiyo, wanafanya biashara hiyo na huwa tunaendelea kuzuia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Watanzania na wafanyabiashara kwamba sera tunayo ya kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara zao kwenye ngazi za chini bila kuingiliwa na watu wa mataifa ya nje na ufuatiliaji huu unabaini haya yote na tunaendelea kuusimamia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa miongozo aliyoitoa kwa ajili ya kuimarisha biashara ndogo nchini na kutengeneza mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara wetu

kufanya biashara kwa uhuru mkubwa kwa ajili ya kupata kipato chao, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa wa Viti Maalum.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mkuu, kutokuzingatia kwa sheria za barabarani na uzembe wa madereva wa bodaboda inatajwa kuwa ni sababu inayosababisha vifo vingi kwa Watanzania wengi hususan vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa.

Je, Serikali ina jitihada gani za makusudi kuhakikisha kwamba vijana wote waliojisajili katika vijiwe wanapata mafunzo sahihi ya usalama barabarani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba tunao wajasiriamali ambao wanaendesha bodaboda ambao wanasaidia sana katika kuchangia pato la Taifa pale ambapo wanafanya biashara zao, lakini pia wanasaidia sana Watanzania kupata usafiri wa haraka wa maeneo mafupi mafupi. Wafanyabiashara hawa wameratibiwa kwenye maeneo mbalimbali, lakini pia wengine wako kwenye vijiwe.

Mheshimiwa Spika, nini Serikali inafanya ili kuondoa au kupunguza sehemu kubwa ya ajali na kuwafanya wafanye shughuli zao kwa usalama?

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Polisi na Usalama Barabarani wanaendelea kutoa elimu kwenye makundi haya ya bodaboda kwenye makundi

ambayo yameratibiwa na yamesajiliwa na kwa miongozo ambayo imetolewa *LATRA* sasa wamepewa mamlaka ya kusajili vikundi vyote vya vijana wa bodaboda ili kuwezesha kuwafikia na kuwapa elimu ya usalama barabarani, lakini pia kuwasaidia katika kufanya biashara zao kwa usalama zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia uko mpango unaoratibiwa na kila halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kuwaanzishia *SACCOS* na ushirika wao mdogo kwa ajili ya kuendesha biashara zao kwa usalama zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea kuratibu kundi hili la madereva bodaboda kwa lengo la kupeleka elimu zaidi, lakini pia kuwaanzishia ushirika mdogo mdogo ambao utaweza kuwasaidia kuchangia fedha na kuwaonesha maeneo ya kupta mitaji na kupanua wigo wa shughuli zao za kibiashara na za usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, pia nitoe wito kwa madereva wetu wa bodaboda popote walipo, ni vema sasa wakaamua kukaa maeneo ambayo yako rasmi na yameainishwa na halmashauri ili iwe rahisi sasa kwa taasisi yetu ya *LATRA* kuwafikia na na kuendesha elimu pamoja na kuwapa fursa mbalimbali za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwahakikishia Watanzania kwamba, eneo hili ambalo limeonekana kuwa na ajali nyingi linaendelea kuratibiwa vizuri kama ambavyo nimesema na Wizara ya Mambo ya Ndani, Kitengo cha Usalama Barabarani kwa lengo la kuwafanya waweze kufanya shughuli zao kwa usalama mkubwa zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwa na kubadilika badilika kwa wakusanyaji wa kodi ya ardhi ndani nchi yetu kwa maana ya Serikali, kuna wakati kodi ya ardhi imekuwa ikikusanywa na TAMISEMI na kuna wakati kodi ya ardhi imekuwa ikikusanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na wakati mwingine kodi hii imekuwa ikikusanywa na *TRA*.

Mheshimiwa Spika, kubadilika badilika huku kwa wakusanyaji wa kodi kumesababisha kukosa ufanisi kwenye makusanyo ya kodi ndani ya nchi yetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inatoa kauli gani kuhusu jambo hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kwagilwa, Mbunge wa Handeni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria tuliyonayo sasa ukusanyaji wa kodi ya ardhi unafanywa na Wizara ya Ardhi yenyewe, Wizara ambayo imepewa mamlaka na Wizara ambayo inafanya kazi ya upimaji wa ardhi, kutoa vibali na inatunza kumbukumbu. Tuliona ni vema na Waheshimiwa Wabunge pia mmechangia pia katika kutunga sheria hii kwamba Wizara ya Ardhi yenyewe ikusanye na sasa tunaona mafanikio ya Wizara hii kukusanya kodi na uelewa wa Watanzania katika kulipa kodi unakuwa mkubwa na kwa hiyo, ukusanyaji unakuwa mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la ukusanyaji wa halmashauri na *TRA*, miaka minne iliyopita hapa tulikutana na Waheshimiwa Wabunge mlitoa ushauri kwa Serikali. haikuwa ni kwa kodi ya ardhi, yalikuwa ni yale malipo ya tozo za nyumba (umiliki wa nyumba) ambayo pia na yenyewe tuliona kuwa ili kupata kodi ya nyumba za ngazi mbalimbali tukabidhi mamlaka iliyoko kule kule ambayo ni halmashauri na *TRA* iko kule kule kwenye wilaya. Kwa hiyo, hawa wakishirikiana pamoja ni rahisi kuzifikia nyumba zao kuliko Wizara ambayo imeishia tu Wizarani na haina tawi kubwa kule kwenye halmashauri. Hiyo ndiyo ambayo tulikuwa tumeipatia halmashauri na *TRA*. Hata hivyo, suala la kodi ya ardhi bado liko chini ya Wizara ya Ardhi na tunaona mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nimpongeze Waziri wa Ardhi kwa kuendelea kufanya maboresho kwenye eneo hili la makusanyo ambako sasa watu wanalipa kielektroniki. Sasa tunaona Watanzania wanapata bili zao kupitia simu zao za mkononi na wanalipa kupitia simu zao za mkononi. Kwa hiyo, makusanyo ya kulipa kodi yanakuwa makubwa kuliko sasa kuliko huko awali ambako tulikuwa tunatumia makaratasi zaidi katika kulipa kodi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania na kuwahamasisha Watanzania kulipa kodi, kodi ndiyo msingi wa maendeleo yetu. Tutakapoendelea kulipa kodi ni rahisi sana kwa Wizara kuratibu mipango mbalimbali ya maboresho ya uratibu wa ardhi kama ambavyo sasa tuna Mradi wa Upimaji wa Matumizi Bora ya Ardhi kwenye vijiji ili kila mmoja aweze kutambua eneo lake na anapotaka kulipa kodi ajue kwamba analipa kodi kwa eneo alilopewa na akiwa na hati yake kamili. Iwe ni hati inayotolewa na Wizara yenyewe au hati ya kimila, zote hizi ni sehemu ya vibali vinavyokuruhusu wewe umiliki ardhi na kukutaka sasa ulipe kodi kwa maendeleo ya Taifa letu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu umekwisha. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Ahsanteni sana, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali ya kawaida, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Athuman Almasi Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na 542

**Hitaji la Gari la Wagonjwa Hospitali ya Wilaya - Uyui**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaipatia Hospitali ya Wilaya ya Uyui gari la wagonjwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imepeleka magari mawili ya kubebea wagonjwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Uyui mwezi Februari, 2024. Magari hayo yamepangwa katika Hospitali ya Wilaya Uyui na Kituo cha Afya Igalula.

Mheshimiwa Spika, magari hayo yanatumika kutoa huduma kwa mfumo wa Kaskedi ambapo Vituo vya Afya vya Loya, Tura, Upuge na Mabama pamoja na zahanati ambazo hazina magari ya kubebea wagonjwa vitahudumiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Athuman Almasi Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, ni lini Serikali itapeleka gari la usimamizi wa huduma katika Halmashauri ya Uyui ambayo ina majimbo mawili Tabora Kaskazini na Igalula?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kutokana na jiografia kati ya vituo hivi vya afya, mfumo wa kutumia gari moja la Kaskedi hautofanya kazi vizuri, je, ni lini Serikali itapanga kupeleka magari

mawili katika Kituo cha Afya cha Upuge na Kituo cha Afya cha Mabamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, magari 70 yaliyokuwa yamebaki ya usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za afya tayari yameingia nchini na Serikali inaendelea na utaratibu wa kuyatoa magari haya bandarini na hatua nyingine za usajili wa haya magari. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba magari haya yakitoka, Halmashauri ya Uyui na yenyewe itapata gari moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie kwamba kama Serikali ilivyotenga pesa kununua magari ya kusafirishia wagonjwa na kuweza kuyaleta katika jimbo lake. Nimhakikishie kwamba Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuongeza magari ya wagonjwa kwa ajili ya kuhudumia katika Vituo vya Afya vya Upuge na Mabamba kama alivyoomba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali moja kwa moja bila historia. Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Serikali tayari imejenga vituo vitatu vya afya katika Tarafa zilizopo Mbulu Mjini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia gari la wagonjwa vituo hivi vyote vitatu vya Jimbo la Mbulu Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kujibu awali kwamba Serikali itahakikisha inatafuta pesa ili iweze kupata magari ya kuhudumia wagonjwa na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kadiri fedha itakavyokuwa inapatika na magari haya kununuliwa, basi yanaweza yakaja kuletwa kwenye vituo vya afya ulivyoomba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, suala la magari linaendana na watumishi wanaohusika kwenye hospitali. Sasa je, ni lini Serikali itapeleka madaktari kwenye Hospitali ya Wilaya ya Chunya maana hospitali nzima ina madakari wawili na mahitaji ni madkatari nane? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekuwa ikitoa vibali vya ajira kwa ajili ya ya kuajiri watumishi katika kada ya afya na kila mwaka imekuwa ikiajiri watumishi hawa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa katika mwaka huu wataajiriwa na katika mwaka ujao wa fedha wataendelea kuajiriwa ili waweze kuhudumia katika vituo vyetu vya kutoa huduma ya afya ya msingi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuipatia Hospitali ya Wilaya ya Tunduru gari la utawala, je, ni lini Serikali itaipatia gari la wagonjwa Hospitali ya Wilaya ya Tunduru? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutafuta fedha za kuhakikisha inanunua magari ya kuwahudumia wagonjwa na kuyapeleka katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma ya afya msingi. Nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kwamba magari haya yakipatikana na yeye ataangaliwa kwa jicho la kipaumbele kwenye jimbo lake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Kitomanga ni miongoni mwa kituo cha afya ambacho hakina magari. Je, kati ya magari hayo 70 Kitomanga itakuwa ni miongoni mwake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kujibu kwenye jibu la msingi kwamba magari 70 ndiyo yaliyokuwa yamebaki na tayari mpaka muda huu yamefika na yapo bandarini yanaendelea na taratibu za kutolewa na kufanyiwa usajili. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba na wao watapata gari hili la usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za afya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mtwango ni kituo cha afya kikubwa sana ambacho kinahudumia Kata ya Kichiwa, Igongolo, Ikuna na Mpakaninga lakini hawana gari la *ambulance* kwa ajili ya wagonjwa. Ni upi mpango wa Serikali wa kupeleka *ambulance* Mtwango?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha inatafuta fedha kwa ajili ya kununua *ambulance*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kadri fedha zitakavyopatikana na magari haya ya kuhudumia wagonjwa yatakaponunuliwa nimhakikishie kwamba Kituo cha Afya cha Mtwango na chenyewe kitapewa mgao wa magari haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Hassan Mtenga.

Na. 543

**Ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya *Masasi DC* na Hospitali Yake**

**MHE. HASSAN S. MTENGA K.n.y. MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza : -

Je, Serikali inaridhishwa na ujenzi unaoendelea wa Ofisi ya Halmashauri ya *Masasi DC* na hospitali yake na juhudi gani zinafanyika kuinusuru?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ni moja kati ya Hospitali 67 zilizoanza kujengwa katika awamu ya kwanza mwaka 2019/2020. Hospitali hiyo mpaka sasa imepokea fedha za ruzuku ya Serikali shilingi bilioni 3.49 ambayo imejenga majengo 15. Aidha, majengo 11 yamekamilika na yanatumika na majengo manne ambayo ni wodi mbili za upasuaji, jengo la kuhifadhia maiti na jengo la upasuaji *(theatre)* yapo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitatu (2020/2021, 2021/2022 na 2023/2024) Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 2.8 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya halmashauri. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 ujenzi wa jengo hilo umefikia 86%. Aidha, miundombinu iliyosalia inategemewa kukamilishwa ifikapo mwezi Septemba, 2024.

Mheshimiwa Spika, jengo la Halmashauri ya Masasi na Hospitali ya Wilaya yameanza kutoa huduma kwa wananchi.

Aidha, majengo yaliyochelewa kukamilika na kuanza kutoa huduma Serikali itaongeza kasi ya ukamilishaji wa majengo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA**: Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa majibu mazuri ya ujenzi huo wa ofisi.

Swali la nyongeza, kwa kuwa Serikali ilitoa fedha nyingi sana kwenye ujenzi huo na majibu ambayo nimeyapata ni mazuri, lakini niiombe Serikali kwa sasa bado hali haijawa nzuri kwenye miundombinu ambayo imebakia.

Je, ni lini Serikali mtaikamilisha ile miundombinu kwa sababu kituo kile tayari kimekwishaanza kutumika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali imeamua kuleta huduma kule chini kwa wananchi, tunayo Kata moja ya Chikongola ambayo ina Kata moja ya Magomeni katika Jimbo la Mtwara mjini ina watu zaidi 29000.

Ni lini Serikali itatuletea kituo cha afya ili kuboresha huduma za afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imefanya tathmini na kubaini kwamba zinahitajika shilingi milioni 883.7 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la utawala, lakini inahitaji milioni 176 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la hospitali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imetengeneza mikakati na ukamilishaji wa majengo hayo yapo katika mpango wa Serikali na Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha inakamilisha majengo haya muhimu.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge linahusu uhitaji wa kituo cha afya kuhudumia idadi kubwa ya wananchi 29,000 nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo lake hili la Mtwara Mjini tayari Serikali imepokea maombi ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati na Mheshimiwa Mbunge na yeye ameleta eneo lake mahsusi ambalo anaona kwamba linahitaji ujenzi wa kituo cha afya na bila shaka eneo hilo kwa kauli ya Mheshimiwa Mbunge ndio hili aliloliombea hapa fedha.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mipango ya upatikanaji wa fedha wa kujenga vituo vya afya vya kimkakati tutazingatia maombi yake ili kituo cha afya kiweze kujengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Bariadi Somanda ni ya kwanza kabisa kujengwa katika Mkoa wa Simiyu lakini haina jengo la *ICU,* ni lini Serikali itatuletea fedha tujenge jengo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kama vile Serikali ilivyoanza kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo mengine katika hospitali hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali imetenga fedha katika mwaka wa bajeti 2024/2025 kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi viporo ya hospitali za halmashauri. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge fedha itakuja kwa ajili ya kuendelea kukamilisha na ujenzi wa jengo hilo *la ICU*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika haina *fence* kwenye majengo yake. Ni lini

Serikali itapeleka fedha kukamilisha ujenzi wa *fence* ya hospitali hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu mkubwa sana wa miundombinu aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kutenga fedha kupitia Serikali Kuu, lakini kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa maana ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kunajengwa uzio huo katika hospitali aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ina nyumba moja tu ya daktari, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza nyumba za madaktari ili watumishi hawa wakae karibu na hospitali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu mkubwa sana wa nyumba za watumishi na hasa katika kada ya afya, Serikali itaendelea kutenga fedha kupitia Serikali Kuu, lakini kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa maana ya mapato ya ndani ya halmashauri kuhakikisha kwamba inajenga nyumba za watumishi ili waweze kuwa karibu na vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi na kuweza kuwahudumia wananchi kwa ukaribu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali fupi.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Myula, Wilaya ya Nkasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kuhakikisha vituo vya afya vyote ambavyo Waheshimiwa Wabunge waliorodhesha kwamba ni vituo vya kimkakati vinaweza kujengwa.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha na kama kituo alichokitaja ni kituo cha kimkakati katika eneo analotoka nimhakikishie Serikali itahakikisha inapata fedha kwa ajili ya kujenga kituo hicho cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, sasa aulize swali lake, Mheshimiwa Kapufi kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge.

Na. 544

**Hitaji la *X – Ray* Vituo vya Afya – Nyang'hwale**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Je, ni lini Vituo vya Afya Kharumwa na Nyang'hwale vitapatiwa *X–Ray*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2023/2024 jumla ya mashine 280 za kidijitali za *x-ray* na mashine za *ultrasound* 322 zimenunuliwa na kusimikwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ilipokea mashine mbili za *x-ray* ambazo zimefungwa katika Hospitali ya Wilaya mwezi novemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za mionzi katika vituo vya kutolea huduma za afya vikiwemo Vituo vya Afya vya Kharumwa na Nyang'hwale.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Vituo vya Afya vya Kharumwa na Nyang'hwale vina uhitaji mkubwa, je, uko tayari kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ili atenge fedha kupitia mapato ya ndani kuweza kujega majengo ya *x-ray machine* hizo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, lini Serikali itapeleka mashine ya *x-ray* katika Manispaa ya Mpanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu *D by D* yaani ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa na zenyewe kutafuta mapato na kuweza kuweka katika mipango na bajeti zake kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali na ujenzi wa miundombinu muhimu. Kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwa na chumba au jengo mahsusi kwa ajili ya matumizi ya mashine hizi za *x-ray*.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumwagiza Mkurugenzi kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mkurugenzi aweze kuweka katika mipango ya kibajeti na waweze kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga majengo haya ili mashine hizi za *x-ray* ziweze kuanza kuwanufaisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, nimhakikishie kwamba katika mwaka wa fedha 2024/2025 serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 66.7 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaweka ombi lako katika kipaumbele ili na wewe kituo chako kiweze kupata mashine ya *x-ray*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, je, ni lini Serikali itapeleka mashine ya *x-ray* katika Vituo vya Afya vya Hirbadau, Mogitu pamoja na Bassotu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 66.7 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wewe vituo vyako hivi vya afya vitakuwa katika mgao wa manunuzi ya vifaa tiba. Kwa hiyo, utapata mashine hii ya *x-ray*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ya *Arusha DC* katika Jimbo la Arumeru Magharibi tumeomba *x-ray* kwa maandishi kupitia Wizara. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka *x-ray* kwenye hospitali hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali imeshatenga bajeti ya vifaa tiba shilingi bilioni 66.7 katika mwaka wa fedha 2024/2025 nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge maombi yake yamepokelewa na yatachakatwa, na yeye atakuwa kwenye mgao wa manunuzi ya vifaa tiba hivi ikiwemo hiyo *x-ray machine*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, vituo vyote sita vya afya katika Wilaya ya Kilwa havina mashine za *x-ray*. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka mashine za *x-ray* katika vituo hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kadiri ya fedha itakapokuwa imepatikana na kwa kuzingatia bajeti iliyopangwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali itaanza kununua vifaa tiba mbalimbali ikiwemo mashine za *x-ray*. Kwa hiyo, wakati wa ugawaji wa vifaa hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaangalia na itaona vipaumbele, lakini itaweza kununua vifaa tiba na yeye atakuwa kwenye mgao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa maelezo aliyoyasema maana yake wilaya nzima haina mashine ya *x-ray?* Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, vituo vyote sita hamna hata kimoja ambacho kina mashine ya *x-ray*.

**SPIKA:** Wilaya nzima haina mashine ya *x-ray* au ni vituo tu vya afya?

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, zipo katika hospitali mbili ya Misheni ya Kipatimu na Hospitali Wilaya ya Kinyonga.

**SPIKA:** Haya hapo sawa basi umeshaeleweka. Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, ni lini Serikali itapeleka *x-ray machine* katika Kituo cha Afya cha Mabamba kilichopo katika Jimbo la Muhambwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA, RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali tayari imeshatenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na kwa kuwa Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 itanunua vifaa tiba, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumepokea maombi yake kwa ajili ya kuona ni namna gani tunaweza tukanunua vifaa tiba ikiwemo hiyo *x-ray machine* aliyoiomba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 545

**Ajira ya Wataalamu wa Mikopo ya Asilimia 10 ya Halmashauri**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaajiri wataalamu wa kuendesha mikopo ya halmashauri ya 10% badala ya kufanywa na Maafisa Maendeleo ya Jamii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiwatumia Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kusimamia na kuratibu utoaji wa mikopo ya halmashauri ya 10% kwa sababu ya utaalamu wao katika shughuli za maendeleo ya jamii. Aidha, wataalamu hawa wamekuwa wakihusika katika kuunda na kusimamia vikundi mbalimbali vya kijamii hususani wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kwa sasa ni kuendelea kuwaajiri na kuwajengea uwezo zaidi Maafisa

Maendeleo ya Jamii pamoja na kuwawezesha kwa kuwapatia rasilimali mbalimbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly Ntate, swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wana utaalamu wa kuanzisha vikundi na kuvisimamia kwa nini wasibaki huko kwenye kusimamia vikundi tu?

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna Maafisa Masoko na Biashara ambao wako kwenye halmashauri na wana utaalamu wa mikopo kwa nini hawa wasisimamie mikopo na kutoa mikopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, vikundi vyetu hivi vinavyoundwa katika halmashauri vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu havijishughulishi na biashara peke yake, lakini vinajishughulisha na shughuli nyingine za miradi kama ya kilimo, ufugaji, utoaji wa huduma za afya, habari na teknolojia. Kwa hiyo hawa maafisa maendeleo ya jamii kazi yao kimsingi ni uratibu na wanashirikiana na wataalamu katika kila sekta wakiwemo hao maafisa biashara, wakiwemo maafisa kilimo, maafisa mifugo, wataalamu wa afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii ni maafisa mahususi kabisa kwa ajili ya kufanya hii kazi, lakini zaidi ya hapo pia umuhimu wa kuwatumia hawa maafisa maendeleo ya jamii ni kwa sababu wapo pia katika kila kata yaani muundo wao wapo katika kila kata na hivi vikundi vinavyoundwa vipo katika ngazi ya kata na vijiji, lakini ukiangalia maafisa biashara wenyewe muundo wao unaanzia katika ngazi ya halmashauri. Kwa hiyo, tafsiri yake hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wanakuwa ni maafisa bora

zaidi na mahsusi kwa ajili ya kufanya uratibu kwa kushirikiana na wataalamu kwa ajili ya kufanya kazi ya vikundi hivi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, sasa aulize swali lake.

Na. 546

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Doma – Mvomero**

**MHE. JONAS V. ZEELAND** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Boma, Kijiji cha Doma, Wilayani Mvomero?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu;-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Doma kipo Kata ya Doma, Kijiji cha Doma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero. Ujenzi wa kituo hiki ulianza mwaka 2021/2022 kwa wananchi kuanza ujenzi wa jengo la huduma za wagonjwa wa nje *(OPD)* ambalo limefikia hatua ya kupandisha kuta.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero imetenga shilingi milioni 40 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya cha Doma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi hasa kwenye vituo vya afya na zahanati zilizopo pembezoni, je, lini Serikali itatuongeza watumishi ili kuweza kupunguza kero hii ya watumishi iliyopo sasa hivi katika vituo vyetu na zahanati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sera ya afya imeweka wazi kwamba kila kijiji lazima kiwe na zahanati na kila kata lazima kuwe na kituo cha afya. Mimi pamoja na wananchi wangu wa Mvomero tumeshajenga maboma zaidi ya kumi, je, lini Serikali itatupatia fedha kwa ajili ya kumalizia haya maboma ambayo tumejenga wenyewe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa watumishi wa kada ya afya katika kuhakikisha huduma bora inawafikia wananchi katika vituo vya kutoa huduma ya afya msingi, tayari Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuajiri watumishi wa kada ya afya na katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali iliajiri watumishi wa kada ya afya 33, mwaka 2022/2023 Serikali iliajiri watumishi wa kada ya afya 36 na mwaka 2023/2024 Serikali imeajiri watumishi wa kada ya afya 48 katika Jimbo la Mvomero.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha inaajiri na kunakuwa na watumishi wa kada ya afya ili waweze kutoa huduma zilizo bora katika vituo vyetu vya kutolea afya msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili ambalo anaeleza kwamba ameweza kuwashirikisha wanchi wake katika kujenga maboma ya zahanati, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali inatambua jitihada kubwa ambayo imefanyika katika ujenzi wa maboma haya na tayari Serikali imefanya tathmini na kubaini kwamba kuna maboma ya zahanati 1,265 ambayo yatahitaji jumla ya shilingi bilioni 75.9 kuyakamilisha.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali imeweka mikakati ya kutafuta na kupata fedha kwa ajili ya kuunga mkono jitihada za wananchi. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali ipo kazini na itahakikisha inatafute fedha ili kujenga maboma hayo uliyoyataja ambayo yako katika jimbo lako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Kata ya Ilangu ni kata ya kimkakati, je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Ilangu Wilayani Tanganyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kutumia mwongozo na maoni ya Waheshimiwa Wabunge Serikali tayari ilishaainisha vituo vya afya vya kimkakati vya kujenga katika kila jimbo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama kituo hiki alichokitaja katika Kata ya Ilangu ni miongoni mwa vile vituo vya afya vilivyoainishwa vya kimkakati nimhakikishie Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha inaenga vituo vya afya hivyo vya kimkakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni lini Serikali itamalizia majengo ya zahanati katika Kijiji cha Iyayi, Uhominyi Nyawegete, Kitoho na Winome ambayo tayari yameshapauliwa na yako katika hatua za umaliziaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inatambua umuhimu sana wa huduma ya afya

msingi na imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha inajenga miundombinu kwa ajili ya kutoa huduma hii ya afya msingi, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kutafuta fedha ili iweze kukamilisha miradi ambayo tayari imeanza ikiwemo mradi alioutaja Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Kabwe kimekuwa kinatolewa kauli tofautitofauti juu ya umaliziaji wake, leo nataka kusikia kwa mara ya mwisho, ni lini mtakamilisha kituo hiki ili kianze kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani kinaitwa nini ili siku nyingine ukiuliza tukukumbushe ulisema leo ni mara ya mwisho.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Kabwe, leo ni mara ya kumi nauliza.

**SPIKA:** Haya Kabwe, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI tayari ilishakusanya vituo vya afya vya kimkakati vya kujengwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 bila shaka Mheshimiwa Mbunge ulileta kituo hiki kukiombea fedha kujengwa katika mwaka wa fedha huu. Nikuhakikishie Serikali inatafuta fedha kuhakikisha kwamba vituo vya afya vya kimkakati katika majimbo yote vinajengwa na kama hiki kituo ni kituo ambacho wewe ulikileta kwamba ni kituo cha kimkakati nikuhakikishie Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona, Kituo cha Afya cha Mji Mdogo wa Makongolosi kimekamilika na kimeanza kutoa huduma, lakini hakina nyumba za madaktari. Chama Cha Mapinduzi Kata ya Bwawani Makongolosi wameanzisha ujenzi wa nyumba za madaktari.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili nyumba hizi za madaktari ziweze kukamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuwapongeza wananchi kwa kushirikiana pamoja kuhakikisha kwamba wanaunga mkono jitihada za maendeleo na kwa kuanza ujenzi wa miundombinu hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama vile ambavyo Serikali imekuwa ikiunga mkono jitihada mbalimbali za kuboresha miundombinu na hasa katika sekta ya afya na kuunga mkono tafsiri yake ni kupitia miradi kutoka Serikali Kuu, lakini pia kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, nikuhakikishie Serikali kwa utaratibu huo huo itaendelea kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana kwa ajili ya kuunga mkono miradi ambayo inaenda kugusa miundombinu muhimu ya afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, sasa aulize swali lake.

Na. 547

**Kutunza Mazingira ya Bwawa la Zombo**

**MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutunza mazingira ya Bwawa la Zombo Kilosa ili litumike kwa shughuli za ufugaji wa samaki na kilimo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza Khamis. Mbona makofi yamekuwa mengi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kutunza mazingira ya Bwawa la Zombo. Hatua hizo ni pamoja na upandaji wa miti kuzunguka bwawa katika eneo la hifadhi ya bwawa ndani ya eneo la meta 60.

Mheshimiwa Spika, aidha katika kipindi cha msimu wa mvua 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kwa kushirikiana na Bonde la Wami - Ruvu, imepanga kupanda miti 5,000 ili kuongeza uoto wa asili na kuzuia mmomonyoko wa udongo katika maeneo yanayozunguka bwawa, aidha kulinda eneo la hifadhi ya bwawa ndani ya meta 60, kuzunguka bwawa dhidi ya shughuli zisizoendelevu na kuendesha doria za mara kwa mara na utoaji wa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa wananchi katika vijiji vinavyonufaika na bwawa husika hususan kilimo na ufugaji, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, bwawa hili limekosa matunzo na hivyo kina chake kimezidi kupungua siku baada ya siku na kusababisha mafuriko katika maeneo ya Miombo, Masanze na Kijiji cha Changarawe.

Je, Serikali ina mpango gani kuokoa maisha ya wananchi hawa kutokana na kadhia ya mafuriko ambayo inatokana na bwawa hili kukosa matunzo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, barabara ya kutoka Mikumi kwenda Kilosa ndani ya kipindi hiki cha mvua imekatika mara nne na kukosa mawasiliano kabisa kati ya maeneo haya mawili kutokana na mafuriko yanayosababishwa na bwawa hili.

Je, Serikali haioni sasa wakati umefika Ofisi ya Makamu wa Rais kukaa na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya kilimo ili kuona namna bora ya kudhibiti mafuriko haya ambayo yanasababishwa na shughuli zisizo endelevu katika Bwawa hili la Zombo maarufu kama Bwawa la Nara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lazaro Londo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii nimshukuru sana na kumpongeza kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwasemea wananchi kwenye jambo hili la mabwawa na mambo mengine ya uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mabwawa mengi hasa kipindi cha mvua yamekuwa yakifurika, yanajaa na ni kweli tumeona mabwawa mengi ambayo tuliyachimba sisi ama yalichimbwa na Wizara nyingine ama taasisi nyingine yamekuwa hayapo kama yalivyokuwa zamani yakiwepo na changamoto za uingiaji wa michanga. Tulichogundua ni kwamba michanga hii inaingia, kwanza ni kwa sababu za shughuli za kibinadamu zinazofanyika zikiwemo shughuli za ufugaji, shughuli za makazi, lakini hata shughuli za kilimo. Kuna watu wanalima karibu na maeneo haya basi michanga inaingia humo mwisho wa siku mabwawa yanafurika halafu yanakuja kuleta shida kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba Serikali tunakwenda kutafuta fedha za kuona namna ambavyo tunaweza tukatoa michanga, lakini pia kuweza kutoa takataka

nyingine ambazo zipo ndani ya mabwawa haya ili kuweza kusafisha na yasiweze kuleta athari.

Mheshimiwa Spika, aidha tunakwenda kushirikiana na Wizara nyingine ikiwemo Wizara ya Kilimo kwa sababu shughuli hizi za uchimbaji zinafanyika, kwa hiyo tutakwenda kushirikiana na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala hili la barabara nimwambie Mheshimiwa tuko tayari kushirikiana na Wizara nyingine ili kuokoa mabwawa haya ili yasijae maji yakafunga barabara au njia yakaleta athari kwa wananchi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, mmekosa maswali kwa sababu aliposimama mwenye swali hamkusimama na ndiyo utaratibu. Anaposimama yeye kuonesha anataka kuuliza la nyongeza na wewe unasimama Spika anakuona. Sasa mmesimama baada, kwa hiyo, mmekosa maswali. *(Kicheko)*

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, sasa auliza swali lake.

Na. 548

**Ujenzi wa Kituo cha Utalii Kihesa Kilolo**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Utalii Kihesa, Kilolo chini ya mradi wa *REGROW?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 26 Januari, 2024 Wizara ya Maliasili na Utalii ilisaini mkataba kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utalii katika eneo la Kihesa Kilolo, Mkoani Iringa kupitia Mradi wa *REGROW*. Aidha, tarehe 27 Januari, 2024 mkandarasi alikabidhiwa eneo la ujenzi na kuanza kazi. Mkataba huo ni wa miezi 12 na unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2025. Hadi kufikia mwezi Mei, 2024 ujenzi wa jengo hilo umefikia 15% na ujenzi unaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza majibu hayo ni kweli kabisa, nawapongeza sana Serikali na mratibu wa *REGROW* Ndugu Saanya pamoja na Wizara kwa kazi kubwa mliyofanya kuanza ujenzi wa kituo hiki, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa moja ya mkakati mkubwa uliotumika kuinua utalii nchini kwa miaka mitatu iliyopita ni kupitia *Royal Tour,* je, ni lini mkakati kama huu utatumika pia ku-*promote* utalii Kusini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, utalii wa vyakula ni moja ya vitu ambavyo watalii wanapenda, ni namna gani Wizara iko tayari kutusaidia kama Manispaa ya Iringa ili tuweze kujikita kwenye utalii wa vyakula hasa ukizingatia kwamba sisi huwa tuna vyakula vingi ambavyo watu wengine kama nyama? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyoneza ya Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza wakati wa bajeti yetu, baada ya uzinduzi wa filamu ya *Royal Tour* tumezindua filamu nyingine inaitwa *Amazing Tanzania.* Sasa hivi tuko kwenye kazi ya ku-*promote* filamu hiyo ili tuweze kuona jinsi ambavyo inaweza kufungua soko la utalii kwenye Bara la Asia. Tutafanyia *monitoring*

ya mafanikio ya filamu hiyo ili tuweze kujipanga kuweza kutangaza maeneo mengine zaidi kupitia filamu za namna hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, katika kukuza utalii wa Nyanda za Juu Kusini tumekuwa na shughuli mbalimbali tunazozifanya, mojawapo ni utalii wa kiutamaduni. Ninawaomba wananchi wa ukanda huu kupitia dirisha hili la utalii wa utamaduni waweze kuendelea kujiunga na kuonesha mahitaji ya kufanya shughuli hii ya utalii wa utamaduni kupitia mambo haya ya chakula ili mradi uweze kuwafadhili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Mradi huu wa *REGROW* ni *package* mojawapo kuhakikisha kwamba wananchi wa Iringa na Nyanda za Juu Kusini wanapatiwa elimu ili waweze kujiajiri kupitia utalii.

Je, ni kwa kiasi gani sasa mmejipanga kuhakikisha wananchi wa Iringa na Nyanda za Juu Kusini wanaopatiwa hiyo elimu ili waweze kuupokea utalii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali lake moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa *REGROW* tayari tunavyo vikundi takribani 600, ni vikundi vya kijamii ambavyo vinatokana na maeneo haya ambayo yana ufadhili wa eneo hili na kumekuwa na ufadhili mbalimbali wa miradi yao kijamii ikiendelea, lakini vilevile tukifanya shughuli ya kutoa mafunzo kwa vikundi hivi ili vifikie mahali ambapo tunaweza kuvifadhili.

Mheshimiwa Spika, nimtoe shaka kwamba tutaendelea na kazi hii ya kutoa elimu. Sasa hivi tunavijengea uwezo vikundi hivi 600, kazi itaendelea. Naomba tuwasiliane ili tuone ni vikundi vya

namna gani viko kwenye maeneo hayo aliyoyasema na tuweze kuviingiza kwenye mpango wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali kwa kifupi, Mheshimiwa Munira.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, ahsante, katika Mradi wa *REGROW* kuna sehemu ya mradi wa uwekezaji wa kijamii ikiwemo vijana katika sehemu inayotekeleza miradi hii. Je, Serikali inaweza kuniambia ni kwa namna gani makundi ya vijana yanafaidika na Mradi huu wa *REGROW?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Munira swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, utaratibu wa mradi huu ni kufadhili vikundi na mpaka sasa tunavyo takribani vikundi 600. Tayari tumeshatoa uwezeshaji au mikopo kwa vikundi visivyopungua 150. Zaidi ya shilingi bilioni tano zimetolewa kwa ajili ya miradi ambayo inaibuliwa na vikundi hivi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge kama kuna kikundi mahususi anadhani hakijaingizwa kwenye utaratibu huu tuweze kushirikiana ili tuweze kuvipatia uwezeshaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, *REGROW Phase One* Kitulo tuliwaacha, *REGROW Phase Two* ni ipi ahadi ya Serikali mtatupatia miradi barabara, miradi ya *accommodation* na uwanja wa ndege? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu tuko kwenye maandalizi, tuko kwenye kukamilisha *REGROW Phase One* lakini vilevile maandalizi ya *REGROW Phase*

*Two,* nimhakikishie tutachukua mawazo yake ili tuweze kuyajumuisha kwenye mchakato wa kuona jinsi ambavyo tutakuja na miradi ya ziada kwenye eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ili kuokoa wakati nikishamtaja Mbunge huna haja ya kumtaja tena, nenda moja kwa moja kwenye majibu. Mheshimiwa Neema Mwandabila swali, la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, kupitia huu Mradi wa *REGROW* natamani kufahamu wana mkakati gani wa kuwekeza kwenye hoteli kwenye maeneo ambayo wanakuwa wamejenga vituo vya utalii, mfano ile *Ngorongoro Reservation* ambayo iko pale Ndolezi, Mkoa wa Songe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, msingi wa *REGROW* ni kujenga mfumo ambao utawezesha kutangaza utalii kwenye maeneo haya. Sasa yapo maeneo ambayo mradi kama mradi unafanya wenyewe, lakini yapo maeneo ambayo tunafanya kutoa chachu kwa sekta binafsi ione umuhimu wa kuja kuwekeza kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa sekta binafsi iliyoko kwenye maeneo haya iweze kujiingiza kwenye utekelezaji wa miradi hii na hata yale maeneo ya hoteli ambayo tunaanzisha bado tutahitaji sekta binafsi ije ishirikiane na sisi kuendeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuko tayari kupokea mawazo yake na baada ya hapa tukae pamoja tuone jinsi gani kuweza ku-*accommodate* mawazo aliyonayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Wilaya ya Kyerwa Kata ya Kamuli ina eneo

linalovutia sana utalii kupitia *hot spring* na ni eneo ambalo hutumika kwa ajili ya kuponya magonjwa, watu wanaweza kutumia yale maji kuweza kupona magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua ni kwa kiwango gani tunaweza kutumia Mradi wa *REGROW* kulitangaza hilo eneo likaingiza fedha kwenye wilaya lakini na Taifa kwa ujumla kwa sababu ni *potential* sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Mradi wa *REGROW* ni kwa ajili ya Nyanda za Juu Kusini, sasa kwa eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema tutawaagiza wataalamu wetu waende wakalione eneo hilo ili tuione fursa iliyopo kwa sababu tunafahamu kwamba maeneo mengi ya namna hii wenzetu wa Wizara ya Nishati wameyaainisha kama maeneo ya kujenga mifumo ya umeme wa joto ardhi. Kwa hiyo, tutaenda kuangalia eneo hilo tuone *potential* iliyopo na tuone ni jinsi gani tunaweza kuliendeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Singida Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 549

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu Singida Kaskazini**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani kuvipatia mawasiliano ya simu vijiji 13 na Kata za Mughunga, Ngimu, Makuro, Mudida, Ughandi, Msisi, Msange na Mgori?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa Kata za Ngimu, Kijiji cha Lamba, Kata ya Msisi Vijiji vya Mnung'una na Mkwae, Kata ya Msange, Vijiji vya Muriga na Endeshi *UCSAF* imeingia makubaliano na *TTCL* kupeleka huduma za mawasiliano katika kata tajwa. Aidha, *UCSAF* pia imeingia makubaliano na *Vodacom* kwa ajili ya kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata ya Ughandi, Kijiji cha Misinko na kwa upande wa Kata ya Mudida, Kijiji cha Migugu *UCSAF* imeingia makubaliano na Kampuni ya Simu ya *Halotel.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa miradi hii, Serikali kupitia *UCSAF* itafanya tathmini ya hali ya mawasiliano katika kata hizo na kuchukua hatua stahiki kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kujua pamoja na kupata hii miradi, lakini utekelezaji wake hadi sasa bado haujafanyika. Kwa hiyo, ni lini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kunihakikishia utekelezaji utaanza?

Mheshimiwa Spika, la pili kuna baadhi ya maeneo mengine ambayo pia yana changamoto ya mawasiliano ikiwemo Kata ya Maghojoa, Kinyagigi, Kinyeto na katika Vijiji vya Minyaa na Kimbii. Ni lini sasa Mheshimiwa Waziri anaweza akanipatia miradi ya minara katika maeneo haya ili wananchi wetu waache kutaabika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ameuliza ni lini utekelezaji utaanza? Tunatarajia mwaka ujao wa fedha maeneo haya yote uliyoyataja Mheshimiwa Mbunge tunakuja kuyafanyia tathmini na kuweza kuyapatia huduma, lakini katika Kata hizi za Kinyeto na kata nyingine ulizozitaja *UCSAF* inakuja kufanya tathmini na lengo ni kuhakiki uhitaji halisi, ni lazima huduma iweze kufikia maeneo haya yote. Kadiri tutakavyopata fedha kuanzia mwaka ujao wa fedha tutahakikisha wananchi nao wanapata huduma nzuri ya mawasiliano. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Naibu Waziri alienda Nyamuhonda, Mwema na Itiryo hakuna mawasiliano kabisa na watu wanasikiliza redio na *Tv* ya Kenya. Ni lini minara itawekwa katika maeneo hayo ili tupate mawasiliano ya Tanzania? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, *UCSAF* inaendelea kufanya tathmini maeneo mbalimbali hasa haya ya mipakani. Mheshimiwa Waitara naomba nikuahidi maeneo haya yote uliyotaja nayo tutayafikia ili waweze kupata huduma ya minara kutoka Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya Mbogwe ina kata 17, Makao Makuu ya Kata ya Mbogwe hakuna mawasiliano na Kata za Nanda, Nhomolwa pamoja na Lulembela na maeneo mengine ya kiuchimbaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Naibu Waziri, ni lini utekelezaji wa minara hii utaenda kujengwa na Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Nicodemas kutoka Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makao makuu ya wilaya na maeneo yanaizunguka yanakosa mawasiliano ya uhakika. Mheshimiwa Mbunge tuko katika mchakato wa kuhakikisha minara inafika maeneo yote muhimu yenye *population* kubwa na pia sehemu za pembezoni. Kwa hiyo, maeneo haya ya Mbogwe pia ni moja ya maeneo ambayo tutawaletea mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize Serikali maeneo ya kwangu maeneo ya Muhanga, Gurungu, Turieli na Mnazi Mmoja pamoja na Kitanula hakuna kabisa mawasiliano, je, Serikali ipo tayari kupeleka minara katika maeneo haya ili wananchi nao waweze kufaidi matunda ya nchi yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahaya kuwa tupo tayari kuleta mawasiliano maeneo haya na tayari michakato ya kuja kufanya tathmini tupo mwishoni kuja kufika maeneo haya yote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, naomba kujua ni lini Kijiji cha Chagu, Kalilani, Songambele na Ikuburu watapata mawasiliano? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mbunge akishatajwa huna haja ya kumtaja tena nenda moja kwa moja kwenye majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunikumbusha.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza katika Kijiji cha Songambele na vijiji vyote ulivyovitaja Mheshimiwa Nashon tunakuja kuleta minara na kuhakikisha mawasiliano yanakuwa murua.

**SPIKA:** Mhehsimiwa Khalifa Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, baadhi ya vijiji vya Jimbo la Mtambwe havina mawasiliano ya simu kabisa. Je, ni lini mtaleta wataalamu wenu kuja kuvitambua na kuvipatia mawasiliano ya simu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza kuwa maeneo ya Mtambwe mwaka ujao wa fedha mapema kabisa wataalamu watakuja kufanya tathmini ili kujua uhitaji ambao unatakiwa katika eneo hili na kuleta mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Mwanza umeendelea kukua kwa kasi na watu wameongezeka na kujenga maeneo ya pembezoni, Serikali ipo tayari sasa kufanya upya tathmini ya mawasiliano na kupeleka minara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, tupo tayari kufanya tathmini mpya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali iliweka minara katika maeneo ya visiwa *base* ambako kulikuwa hakuna mawasiliano, sasa hivi mawasiliano wanapata, changamoto waliyonayo hawana zile *voucher* za kukwangua na si wote waliozoea kununua kwa kutumia simu. Ni lini *voucher* hizo zitapatikana ili mawasiliano yao yawe mazuri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Najiuliza kama swali la *voucher* ni la Serikali au ni la yale makampuni labda hakuna biashara huko? Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kuhusu vocha za kukwangua, naomba niseme nimelipokea nitalifikisha kwa watoa huduma lakini kama Serikali tunaendelea kutaka kuboresha kuondokana na hizi *hard copies* na kuingia kwenye *voucher* moja kwa moja kupitia mtandao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kiwombi - Kata ya Amanimakoro, Kijiji cha Sala - Kata ya Muhongozi, Kijiji cha Kihangimauka - Kata ya Kihangimauka, vijiji hivi vilikuwa na makubaliano na *UCSAF* lakini hadi leo hakuna kinachoendelea. Ni lini minara hii inaenda kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nikupongeze Mheshimiwa

Mbunge hili suala tumeliongea jana tu na tumeshakubaliana mimi na wewe tutakwenda, lakini nimeshatoa maagizo kwa Meneja wa Kanda Nyanda za Juu Kusini anashughulikia hii minara. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali.

Mheshimiwa tafuta kiti uketi.

Waheshimiwa Wabunge, nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele tutaanza na tangazo la wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika, kwanza ni wageni wangu ambao ni Taasisi ya Tanzania-*China Friendship Promotion Association* hapo yupo Mheshimiwa Balozi Jiang Jiang ambaye ni Makamu wa Rais wa Chama cha Watu wa China cha Kukuza Urafiki na Nchi za Kigeni, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ameongozana na Ndugu Zhang Rong ambaye ni Mkurugenzi, Idara ya Masuala ya Asia na Afrika, karibu sana. *(Makofi)*

Pia ameongozana na Ndugu Huang Xiaowei ambaye ni Mkurugenzi, Idara ya Masuala ya Asia na Afrika, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Joseph Kulwa Kahama ambaye ni Katibu Mkuu wa Taasisi ambaye yeye ni mwenyeji, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wangu wengine ambao ni Kikundi cha Sauti ya Mwanamke kutoka Mkoa wa Mbeya na hawa ni Ndugu Lilian

Mwakitosi, Ndugu Miriam William, Mheshimiwa Atupele Msai, huyu ni Diwani, yupo Ndugu Tatu Mbamba, Ndugu Juliana Kibasa, Ndugu Tumaini Mwakasege huyu ni Mjumbe wa Baraza la UWT, lakini pia yupo Ndugu Margaret Benedict, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wenu mbalimbali ambao wapo pia hapa Bungeni, tutaanza na wageni 150 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Maskauti kutoka Shule ya Msingi na Sekondari Tusiime na Shule ya Msingi Michael Mausa za Ilala, Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa ambaye ni Naibu Waziri wa Madini, hawa ni wapiga kura wake pamoja na mke wake kutoka Longido Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Hebu mke kwanza, mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri, haya ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati ambaye ni kada wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Kilolo, Mkoa wa Iringa, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete ambao ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Tarime, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Tunao Wageni watatu wa Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika ambao ni Waandishi wa Habari wa *King's FM Radio* na *Uplands FM* kutoka Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, taarifa za ziada nilizoletewa hapa kwamba *King's FM* inamilikiwa na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, kwa hiyo tunawakaribisha sana, lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo aliwatambua kama sehemu ya vyombo vya habari ambavyo vinachangia sana katika kuzungumza kuhusu maadili bora katika jamii. Tunawakaribisha sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Juliana Shonza ambao ni wadogo zake kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mhehsimiwa Sebastian Simon Kapufi ambao ni wanafunzi waliosoma Shule ya Sekondari Kazima, Mkoa wa Tabora miaka ya 1980 na 1990, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tutaanza na Bi. Rahabu Mwakatungila mjasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi saba kutoka *St. Mary Goreti Secondary School* ...

Mheshimiwa Anatropia nimesimama bado.

Tunao wanafunzi saba kutoka *St. Mary Goreti Secondary School* ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 18 wa Shule ya *Kisiwani English Medium* kutoka Jijini Mwanza, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia tunao wanafunzi 45 na walimu watano wa Shule ya Msingi *Shree Hindu Mandal* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo pia tangazo linalotoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo tutakuwa na kikao mara baada kusitisha Shughuli za Bunge, ikiwa tutasitisha saa 7.00 mchana basi tutakutana saa saba Wabunge wanawake wote. Kama tutasitisha kabla ya hapo basi mara baada ya kusitisha

Shughuli za Bunge tutaonana Ukumbi wa Spika uliopo jengo la utawala, ghorofa ya tano.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa mujibu wa Kanuni ya 76, mapema leo wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anajibu maswali na hasa swali la Mheshimiwa Lucy Mayenga, alipokuwa anazungumza namna ambavyo biashara inafanyika hasa na watu kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Tarime Vijijini, eneo langu limeathirika sana na kadhia hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameizungumza hapa. Sasa hivi wananchi wangu wakilima viazi wale wenzetu wa Kenya wanaenda mpaka vijijini kwenye vitongoji kuchimba kwenye mashamba, ndizi zinakatwa hata kabla ya kukamilika, akina mama pale Sirari na masoko mengine walikuwa wameweka vibanda vyao wanauza mchele, leo wale watu wanafuata mchele, kwa hiyo wale akina mama wamefunga maduka yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba katika jambo hili kwa kweli watu wetu wameathirika sana. Tunapenda wageni, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla ni muhimu watoe mwongozo kwamba ni biashara gani wageni wanaweza kufanya na wananchi wa kawaida wafanye biashara gani ili wasiathirike, tuna wakati mgumu sana watu wa karibu na Mkoa wa Mara na maeneo mengine ya jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeomba Mwongozo wako juu ya jambo hili. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelezo lakini kwa namna ilivyo Tarime leo, hali ni mbaya kweli kweli na

wananchi wanalalamika sana. Tumewahamasisha wananchi walime *avocado* yale, yanachumwa hata madogo kabisa kwenye mashamba yao na kwenda kuyavundika kwa hiyo hatunufaiki na biashara ile.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, ni jambo gani hapo unataka litolewe Mwongozo na Kiti?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ninachoomba hapa ni kwamba pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu huo Mwongozo ni sehemu ya utaratibu wa kufanya biashara, watu wa nje ya nchi kuingia na kufanya biashara mbalimbali katika maeneo yetu hauna Mwongozo huo, wananchi hawajui. Hata Wenyeviti wa Vijiji hawana Mwongozo na hawana Sheria.

Kwa hiyo, utolewe utaratibu wa Kiserikali kwamba, wananchi waambiwe kama ni mazao ya biashara ni yapi ambayo wanaweza kufanya wageni na vibali vinatolewa namna gani ili wao waweze kunufaika katika biashara ile. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijajibu huu Mwongozo wa Mheshimiwa Mbunge kuna wageni hapa mniwie radhi nilikuwa nimeruka kuwatangaza.

Wageni 28 wa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga ambao ni Makatibu Kata na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, amesimama hapa Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara akitaka nitoe Mwongozo juu ya jambo ambalo limetokea hapa Bungeni ambalo Mheshimiwa Lucy Mayenga ameuliza swali na likajibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Sasa maelezo aliyotoa Mheshimiwa Mbunge kwa sababu wote tumeyasikia sitayarejea hayo, lakini anataka kujua kama

jambo hilo alilolisema linaruhusiwa ama haliruhusiwi na Mwongozo huo unaombwa kwa jambo lililotokea hapa ndani siyo lililotokea nje ya hapa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alichojibu kinaruhusiwa, kwa mujibu wa Kanuni zetu majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa swali alilokuwa ameulizwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga, yanaruhusiwa. Kwa hiyo, huo ndiyo Mwongozo wangu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilisema baada ya matangazo hayo, tutaendelea na ratiba yetu. Sasa nimwite Katibu kwa ajili ya ratiba inayofuata.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA BINAFSI ZA WABUNGE

### Hoja kuhusu Halmashauri za Miji na Wilaya Kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Kutatua Tatizo la Upungufu wa Magari ya Zimamoto pamoja na Vifaa Vinavyotumika Kuzima Moto na Uokoaji

**SPIKA:** Tunayo Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, sasa nimwite awasilishe hiyo hoja yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Prisccus Jacob Tarimo. *(Makofi)*

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na hatimaye kutukutanisha tena katika Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi na Mbili tukiwa wazima wa afya.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukupongeza kwa dhati kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mabunge Duniani na kwa namna unavyoliongoza Bunge letu Tukufu kwa viwango vya hali ya juu. Kuchaguliwa kwako kumeiletea heshima kubwa nchi yetu na Bunge letu duniani. Aidha, uongozi wako imara umetuwezesha

kutekeleza majukumu yetu ya kuisimamia Serikali na kuishauri ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(2) na 61(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilihisha Hoja Binafsi katika Bunge lako Tukufu kuhusu Halmashauri za Miji na Wilaya Kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Kutatua Tatizo la Upungufu wa Magari ya Zimamoto pamoja Vifaa Vinavyotumika Kuzima Moto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu inakusudia kuitaka Serikali kuziruhusu halmashauri hizo kuingia makubaliano na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji *(MoU)* ili kuziwezesha kukabiliana na tatizo lililopo nchini la kuwepo kwa upungufu wa magari ya zimamoto na vifaa vya zimamoto na uokoaji katika baadhi ya halmashauri. Vilevile kukabiliana na upungufu katika utoaji wa huduma za zimamoto na uokoaji.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005 inaeleza kuwa Serikali maana yake ni pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Serikali za Mitaa na pia mtu mwingine anayetekeleza madaraka au mamlaka yoyote kwa niaba ya Serikali. Aidha, Katiba yetu inaeleza kuwa lengo la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi na pia imefafanua kwamba Serikali itawajibika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Serikali inatimiza lengo la kuendeleza, kuhamasisha na kukuza ustawi wa wananchi, Serikali za Mitaa zimeanzishwa chini ya Katiba yetu katika mikoa, wilaya, miji na vijiji ambazo kwa mujibu wa sheria zimepewa jina la halmashauri kwa madhumuni ya kupeleka madaraka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, halmashauri hizo zimepewa haki na mamlaka ya kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli mbalimbali za utekelezaji wa maendeleo katika halmashauri husika. Hali kadhalika, halmashauri zimepewa mamlaka ya

kusimamia utekelezaji wa sheria na wananchi wanapata huduma ya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha halmashauri zinadumisha ustawi na usalama wa wananchi katika maeneo husika, zimepewa mamlaka ya kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato na kutumia mapato hayo kutekeleza kazi za umma katika halmashauri. Kiutaratibu, fedha za halmashauri kwa kuwa zinahusika katika kutekeleza miradi ya eneo husika zimepewa jina la fedha za ndani. Fedha kutoka Serikali Kuu zinafahamika kama fedha kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuweza kusimamia vyema Sera ya Ugatuzi wa Madaraka kwa kuhakikisha Serikali za Mitaa zinakusanya fedha kutoka katika vyanzo vilivyopo katika halmashauri husika na kuruhusu halmashauri hizo kuzitumia kwa ajili ya kuendesha miradi iliyopo. Uamuzi huu umewezesha wananchi kuiona thamani ya pesa ya Serikali moja kwa moja na utaratibu huo unasaidia sana katika kupunguza utegemezi wa fedha kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, licha ya halmashauri kuruhusiwa kutumia fedha hizo kutoka vyanzo vilivyopo kwenye eneo husika katika kutekeleza miradi iliyopo kwenye maeneo yao bado yapo baadhi ya masuala ambayo halmashauri hazina mamlaka ya moja kwa moja katika kupanga na kutenga bajeti ya mambo inayoona ni muhimu kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya masuala ambayo halmashauri za miji na wilaya nchini zinashindwa kuyatekelezea katika muda ambao halmashauri inaona inafaa, ni ununuzi wa magari ya zimamoto na vifaa mbalimbali vinavyotumika katika kuzima moto na uokoaji. Ugumu huo unatokana na halmashauri kushindwa kutumia fedha zake za ndani kutekeleza miradi husika kutokana na misingi ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 2007 masuala yote ya huduma ya zimamoto na uokoaji yalikuwa yanasimamiwa kwa ukaribu na Serikali za Mitaa kupitia halmashauri za miji na wilaya.

Halmashauri hizo husika zilihusika kikamilifu katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za zimamoto na uokoaji kwa kutenga bajeti kuhusu masuala yanayohusu ununuzi wa magari ya zimamoto pamoja na vifaa vya uokoaji.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, mwaka 2007 tangu wakati huo hadi sasa masuala yanayohusu ununuzi wa magari ya zimamoto na vifaa vya uokoaji yanafanyika na Serikali Kuu kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Aidha, tangu jukumu hilo kuhamishwa katika jeshi hilo, kumeendelea kuwepo na upungufu mkubwa wa magari na vifaa vya zimamoto na uokoaji katika halmashauri nyingi kwa kuwa Serikali Kuu hukosa fedha za mkupuo kununua magari hayo kwa halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo hilo limesababisha Waheshimiwa Wabunge wengi kuuliza Serikali mara kwa mara maswali kuhusu kuwepo kwa magari ya zimamoto, ubovu wa magari ya zimamoto, umbali mrefu kutoka magari ya zimamoto yalipo hadi maeneo ambapo majanga yanatokea na kutokuwepo kwa vifaa toshelezi vya kisasa vya zimamoto na uokoaji.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya Waheshimiwa Wabunge wote ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya zimamoto na uokoaji kwa haraka na kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005, Ibara ya 147(1) na (2) na Ibara ya 148(1), inaeleza madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu kuunda jeshi la aina yeyote na kuyaamuru majeshi hayo katika kuokoa maisha na mali ya watu katika hali ya hatari na hapo ndipo Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilipoundwa kwa lengo kuu la kuokoa maisha na mali.

Mheshimiwa Spika, aidha, sina shaka na uhodari na uwezo wa askari wa jeshi hili, bali wanahitaji vifaa vya uokoaji na magari ya kuzima moto ya kutosha katika kutimiza majukumu yao ya kisheria na Kikatiba katika kuhakikisha usalama wa wananchi. Serikali Kuu ibakie na jukumu la kutoa maafisa na askari wetu

hodari na wazalendo, lakini halmashauri hizi ziweze kushiriki jukumu la uwekezaji wa miundombinu wezeshi ikiwemo magari ya zimamoto na vifaa katika shughuli za uokoaji nchini.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali kwa maswali hayo kwa Waheshimiwa Wabunge ni kuwa Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inafanya kazi kubwa na imetenga bajeti ya kununua idadi ya magari husika. Idadi ya magari ambayo Serikali inaeleza kuyanunua ni ndogo sana ukilinganisha na mahitaji yaliyopo kwa kuwa idadi ya halmashauri zinazohitaji huduma hiyo ni kubwa sana ukilinganisha na idadi ya magari na vifaa vya uokoaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, uwezekano wa kukabiliana na majanga ya moto na ajali nyingine utaendelea kuwa mgumu kutokana na kukosekana kwa magari na vifaa vya uokoaji.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka ya karibuni, ajali na majanga ya moto yameendelea kuongezeka kwa kasi kubwa katika maeneo ya wananchi katika miji, katika vijiji mbalimbali nchini. Mji wa Moshi ambao ni jimbo ambalo mimi ni mtumishi wao, ni mfano mzuri mmojawapo ambapo majanga makubwa mawili ya moto yalitokea ndani ya muda mfupi katika siku za karibuni katika soko la Mbuyuni.

Mheshimiwa Spika, katika matukio yote hayo, uwezo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kukabiliana na majanga haya umekuwa mdogo kabla haujaleta madhara zaidi na kufanya uokoaji kuwa mgumu. Kukosekana kwa ufanisi wa uokoaji unasababishwa kwa sehemu kubwa na upungufu wa magari ya zimamoto na vifaa vya uokoaji.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoji lina jukumu la utoaji wa elimu, upitishaji wa ramani za majengo na ukaguzi wa majengo. Lengo la jukumu hili ni kuzuia majanga ya moto yasitokee, kupunguza athari za majanga endapo yatatokea na kujenga uwezo wa jamii namna ya kukabiliana na majanga hayo. Kimsingi tunaposema jeshi linapaswa kuwa *proactive* maana yake ni jukumu hili linapaswa kupewa kipaumbele, hivyo matokeo

chanya ya kutekeleza majukumu haya ili kupunguza kwa matukio ya moto na maokozi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jukumu hili muhimu la uokoaji na uwepo wa jeshi na askari wengi ili kupata majengo yote kukaguliwa na kutoa elimu na ushauri wa kinga dhidi ya majanga ya moto.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na utokeaji wa majanga mbalimbali yaliyoletea maafa kwa wananchi yakiwemo maporomoko ya udongo kule Hanang, Mkoani Manyara, mafuriko katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na hata Moshi.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya mwaka 2022, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni mojawapo ya Wajumbe wa Kamati ya Wataalamu wa Kitaifa na idara zinazohusika na huduma za masuala ya maafa katika uokoaji wa maisha na mali. Hata hivyo, idadi ya askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika matukio haya ni ndogo sana ukilinganisha na idadi ya waathirika wa majanga na kushindwa kutoa huduma hii kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaokumbwa na majanga wamekuwa wakitoa lawama kwa halmashauri kwa kudhani kwamba kukabiliana na majanga hayo ni jukumu la halmashauri. Aidha, wanaona kuwa halmashauri inao wajibu wa kununua vifaa toshelezi katika kukabiliana na majanga katika maeneo husika. Vilevile halmashauri zimeendelea kulaumiwa kwa kukusanya mapato kutoka kwa wananchi, lakini zimekuwa haziwasaidii kuepukana na majanga ya moto mfano katika masoko na maduka na maeneo ya biashara, hali hii husababishwa na halmashauri kutopewa jukumu la kuwekeza katika ununuzi wa vifaa hivi.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya miji, wahisani na wadau wa maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi walikuwa wakizisaidia halmashauri kukabiliana na majanga hayo, mfano mojawapo ni

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ambayo ilishapewa magari na miji marafiki kutoka Japan kwa ajili ya kuzima moto.

Mheshimiwa Spika, baada ya majukumu hayo ya ununuzi wa vifaa vya zimamoto na uokoaji kuhamishiwa Jeshi la Zimamoto, hata vile vifaa ambavyo halmashauri zilikuwa zimepewa, zilihamishiwa kwenye Jeshi la Zimamoto. Halmashauri zimeshindwa kuendelea na mawasiliano kwa wahisani na wamekuwa wakiona ugumu kwa wahisani hao kutoa misaada ya ununuzi wa vifaa hivyo kwa halmashauri kutokana na kwamba vifaa hivyo sasa vimehamishiwa kwenye Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na miradi mikubwa ya kimkakati kama vile *Standard Gauge Railway (SGR)*, *Julius Nyerere Hydroelectric Power*, Bomba la mafuta la Uganda na Tanzania, lakini miradi hii mikubwa inategemea huduma ya zimamoto na uokoaji kutoka katika vituo vya zimamoto na uokoaji vilivyo mijini ambapo ni mbali na eneo lilipo. Hata hivyo, miradi hii inahitaji huduma ya zimamoto na uokoaji kwani inaweza kupata hitilafu na kutokea ajali ya moto na majanga mengine na pengine kukwamisha miradi hii kuendelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kupitia *CSR*, miradi ikiruhusiwa kujenga vituo na ununuzi wa magari ya zimamoto na uokoaji, vitasaidia kusogeza huduma hii kwa miji iliyo karibu na eneo ambapo miradi hiyo ilipo iwapo itatokea dharura ya majanga, itadhibitiwa kwa haraka kabla haijaleta maafa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kiuhalisia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina vituo vichache sana vya kutoa huduma kwa wananchi, hali hii imesababishwa na upungufu wa rasilimali vifaa na rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto tajwa, mara kadhaa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amekuwa akizielekeza Halmashauri zote nchini kutenga maeneo ya kujengwa vituo vya zimamoto na uokoaji na kununua vifaa ikiwemo kukarabati magari na kukabidhi Jeshi la Zimamoto

na Uokoaji ili kusogeza huduma kwa wananchi na kuboresha huduma kwa halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hilo, Halmashauri ya Mji wa Tunduma imekuwa ya kwanza kununua gari la zimamoto na kukabidhi kwa Jeshi la Zimamoto kwa matumizi ya halmashauri hiyo. Itakumbukwa kuwa kabla ya huduma za zimamoto na uokoaji kutolewa chini ya Kamandi moja ya Kamishna Jenerali, huduma tajwa zilitolewa katika ngazi ya halmashauri ambapo halmashauri iligharamia mishahara, *uniform*, posho na ununuzi wa magari na vifaa vya uokoaji.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, kwa sasa halmashauri zimepunguziwa mzigo wa kugharamia huduma hiyo. Hivyo, unafuu huo unaweza kuzirudishia halmashauri jukumu la kushiriki katika kununua magari na vifaa vya uokoaji kwa ajili ya kuboresha huduma katika halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni upatikanaji wa maji wakati wa ajali za moto kwani *fire hydrants* ni chache sana katika miji, aidha, Jeshi lishirikiane na Wizara ya Maji pamoja na Mamlaka za Maji na wadau wengine, kuwe na ulazima kunapokuwa na miradi mipya ya maji wazingatie uwekaji wa sehemu za kujazia maji ya zimamoto *(fire hydrants),* pamoja na kufanya matengenezo ya *fire hydrants* zilizoharibika au kufukiwa wakati wa matengenezo ya barabara ili ziweze kutoa huduma na kuokoa maisha na mali.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu inalenga kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuwasajdia wananchi katika kukabiliana na majanga kwa kuingia makubaliano maalum *(MoU)* kati ya halmashauri na Jeshi la Zimamoto katika kununua magari ya zimamoto na vifaa vya uokoaji kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika halmashauri husika na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liwe na kazi moja tu ya kuleta maafisa na askari katika vituo vyote vya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa halmashauri ni Serikali ambayo lengo lake kuu ni kujenga, kuimarisha na kukuza ustawi wa

wananchi, na kwa kuwa halmashauri pia zina wajibu wa Kikatiba katika kuhakikisha usimamizi wa sheria na ulinzi wa wananchi, ninapendekeza halmashauri za miji, wilaya ziruhusiwe kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili kuziruhusu halmashauri kununua magari ya zimamoto, vifaa vya uokoaji na kufanya ukarabati wa kawaida *(maintenance)* wa magari na vifaa hivyo katika kukabiliana na tatizo la upungufu na ukosefu wa magari na vifaa hivyo katika halmashauri nchini ikibidi kwa kuingia makubaliano maalumu *(MoU)* pamoja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuliomba Bunge lako Tukufu lijadili hoja hii na liazimie kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa lengo la Serikali ni kujenga, kukuza na kuimarisha ustawi wa wananchi kwa kutatua matatizo yanayowakabili ikiwemo kutekeleza miradi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ni halmashauri za miji, manispaa, wilaya, kata na vijiji;

Na kwa kuwa halmashauri zinaruhusiwa kubuni vyanzo vya mapato kutoka katika maeneo husika, kukusanya mapato na kuyatumia katika kutatua changamoto zinazowakabili wananchi ikiwemo ujenzi wa masoko, miradi ya maji, hospitali, majengo mbalimbali, shule, magari na vifaa mbalimbali ikiwemo vifaa vya usafi na ulinzi;

Na kwa kuwa yamekuwa yakitokea majanga ya moto na ajali nyingi katika maeneo mbalimbali katika halmashauri za miji, manispaa, wilaya, kata na vijiji na kuna uhaba wa askari wa zimamoto na uokoaji nchini ingawa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linahusika kisheria katika kuokoa maisha na mali za wananchi pale majanga yanapotokea;

Na kwa kuwa majanga ya moto na ajali yameendelea kuleta madhara makubwa kwa wananchi kwa kuharibiwa mali, kupata vilema vya muda na vya kudumu, madhara ya kiafya wakati mwingine kusababisha vifo vya wananchi;

Na kwa kuwa kwa sehemu kubwa ya ukosefu wa magari ya zimamoto na vifaa vingine vya uokoaji katika halmashauri mbalimbali nchini inachangia ongezeko la madhara yatokanayo na ajali za moto na ajali nyingine kwa kukosekana ufanisi katika huduma ya kuzima moto na uokoaji kukabiliana na majanga hayo;

Kwa kuwa baadhi ya halmashauri zinao uwezo wa kifedha wa kuwezesha kupatikana kwa magari ya zimamoto na vifaa vya uokoaji katika kuhakikisha usalama wa wananchi na mali zao kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

Na kwa kuwa hakuna makubaliano kisheria kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kushirikiana na Mamlaka za Maji kwenye umiliki, uwekaji na ukarabati wa *fire hydrants* kupitia miradi mipya ya maji na ya zamani nchini;

Kwa kuwa sheria inayosimamia masuala ya zimamoto na uokoaji haitoi mwanya kwa halmashauri kununua magari ya zimamoto na vifaa vingine vya uokoaji kutokana na jukumu hilo kuwa chini ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

Na kwa kuwa baadhi ya halmashauri zinao uwezo wa kibajeti na uwezo wa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika kutatua changamoto ya upungufu wa magari ya zimamoto na vifaa vya uokoaji kupitia vyanzo vya mapato ya ndani, msaada kutoka kwa wahisani, marafiki na wadau wa maendeleo ama fedha kutokana na utekelezaji wa sera ya huduma za kijamii *(CSR*) kutoka kwa wadau mbalimbali;

Na kwa kuwa Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge la Jamhuri ya Muungano linayo mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika utendaji wake wa kazi.

Kwa hiyo basi, ninaomba Bunge liazimie kwamba:-

(a) Serikali ilete Muswada wa Sheria Bungeni ili kuweka utaratibu wa kuwezesha halmashauri kutenga fedha

katika bajeti zake kwa ajili ya kununua magari ya zimamoto, vifaa vingine vya uokoaji na matengenezo ya magari na vifaa vya zimamoto na uokoaji;

(b) Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria utakaoweka utaratibu wa kuwezesha halmashauri za miji na wilaya kuingia makubaliano ya ushirikiano *(MoU)* na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya kununua magari ya zimamoto na vifaa vya uokoaji;

(c) Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria utakaoweka utaratibu wa utekelezaji wa sera ya huduma kwa jamii *(CSR)* kuwezesha miradi mikubwa ya kimkakati kuweka huduma za zimamoto na uokoaji;

(d) Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria utakaoweka utaratibu wa kuwezesha uwekaji wa *fire hydrants* katika miradi yote ya maji na kuingia makubaliano ya ushirikiano *(MoU)* kati ya Mamlaka za Maji nchini na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika uwekaji na ukarabati wa *fire hydrants;* na mwisho

(e) Serikali iweke utaratibu maalum wa kuwezesha upatikanaji wa ajira kwa Jeshi la zimamoto na uokoaji kuajiri Askari wengi kila mwaka ili kukidhi shughuli za uokoaji na kupambana na majanga nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana, tunaweza sasa kuketi. Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba

kuchangia hoja hii. Nasikia watu wanasema haa! Kanuni zetu zinasema namna ya kuomba kuzungumza humu Bungeni, njia mojawapo ni ya kusimama uonwe, njia ya pili ni wewe kumjulisha Mheshimiwa Spika.

Kwa hiyo, wale walionijulisha ninayo majina yao hapa. Sasa watu naona wanafanya haa, kama vile lazima, kama vile hawajazipitia Kanuni zetu.

Waheshimiwa Wabunge, naona mnaendelea kuchomoza kama…, naona kila mmoja anaendelea kuchomoza hapa. Watafanikiwa Wabunge wachache kwa sababu ya majina niliyonayo hapa, lakini pia na muda ambao tumetenga kwa ajili ya hoja hii binafsi ya Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo wataongezeka wachache wale waliosimama. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Abdallah Chikota, leo umeuliza swali la nyongeza, si ndiyo? Enhee! keti.

Mheshimiwa Martha Mariki umeuliza swali la nyongeza leo, Mheshimiwa Stanslaus Mabula umeuliza swali, Mheshimiwa Kanyasu, haya. Wengine ni Mheshimiwa Tarimba, Mheshimiwa Neema Mwandabila umeuliza swali leo, keti. Mheshimiwa, eeh, wa Dar es Salaam na Pwani mbona wamesimama wengi, siyo awawakilishe mmoja? Haya, ndiyo wanaongoza kwa majanga? Haya, ahsante sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwakamo, Mheshimiwa Mtemvu, Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi, Mheshimiwa, ngoja, Mheshimiwa Kwagilwa, umezungumza leo? Keti, umeuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, siyo?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ninatoka kwenye eneo ambalo lina Mradi wa Kitaifa Msomera. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahaa, ngoja. Tunatoa vipaumbele, sasa tutafanyaje? Maana muda ndiyo huu huu.

Haya Mheshimiwa Maganga si uliteta ujumbe tayari ama unataka Kanuni moja itumike mara mbili? Mheshimiwa Ally Kasinge, Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma Mjini - Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mheshimiwa Anatropia umeuliza swali la nyongeza labda akisimama mwingine upande huu, haya hakuna.

Kwa hiyo, sawa naam ahaa, wameshaleta majina? Haya mmeishaleta majina kwa hiyo yako hapa tayari. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hawa watapata nafasi ya kuchangia na nadhani tuchangie dakika tano, haya naambiwa hata mbili, tano ambaye hatamaliza atakuwa ametusaidia. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Maganga na Mheshimiwa Felista Deogratius Njau ajiandae.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii nichangie hoja binafsi ya Mheshimiwa Tarimo.

Mheshimiwa Spika, kwenye hoja hii naomba niwe *clear,* ninaunga mkono baadhi ya *items* kwenye hoja, lakini siungi mkono *general* ya hoja nzima, nadhani nimeeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaungana mkono na Mheshimiwa Mbunge kwamba Jeshi letu la Zimamoto linakabiliana na changamoto nyingi na kwa mfano pia kwenye jimbo langu hivi karibuni tumepata majanga mawili ya moto lakini kutokana na changamoto ambazo ziko Jeshi letu la Zimamoto, changamoto hizo zimeshindwa kuhudumiwa kwa wakati unaostahili kuna basi liliungua Zimamoto hawana gari la kuzimia moto, lakini hawana askari wa kutosha lakini kuna nyumba ya mwananchi wangu iliungua. Kwa hiyo, ninamuunga mkono Mheshimiwa Tarimo kwamba Jeshi letu lina changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ambazo zinakumba Jeshi letu la Zimamoto, moja ni upungufu wa askari wake, mbili, mitambo ya kuzimia moto, tatu, *fire hydrants* au vituo vya kujazia maji, ya nne upungufu wa magari ya *administration*, tano, ujenzi holela, sita *fire detector* huko mitaani.

Mheshimiwa Spika, hata kama tuna hizi changamoto sioni kama ni busara kuiongezea halmashauri zetu jukumu hili kubwa na zito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ipo, lakini sioni kama ni busara jukumu hili zito kulipelekea halmashauri zetu, lakini kama kuna halmashauri zinao uwezo wa kununua magari ambapo kuna baadhi ya halmashauri zimekwishakufanya hivyo, basi zifanye hivyo. Kama kuna watu binafsi au kuna taasisi ambazo zinaweza kusaidia Jeshi letu la Zimamoto zifanye hivyo kuliko kuongezea halmashauri zetu kazi hii kubwa ambayo hawataiweza na pia hii ni kazi ya kitaalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nitumie muda huu wa kwangu uliobaki kuipongeza Serikali yetu kwa namna inavyopambana, dakika zangu tano bado.

Mheshimiwa Spika, moja tunashukuru Serikali yetu kupitia Jeshi letu la Zimamoto linakabiria kupata fedha zaidi ya dola milioni 100. Fedha hizi zinaenda moja kununua magari zaidi ya 150, fedha hizi zinaenda kununua helikopta, fedha hizi zinaenda kununua boti kwenye bahari zetu na maziwa yetu ambayo vifaa hivi vitaenda kuongezea nguvu kwenye Jeshi letu la Zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuzidi kulipa nguvu Jeshi la Zimamoto ili liweze kupambana na majanga haya kuliko kuchukua majukumu yake na kuwapa halmashauri ambayo kitalamu hawana uwezo, hawana watalamu wa kuweza kufanya hivyo, wakati tuna Jeshi ambalo lina watu wako *trained,* tuna Jeshi ambalo lipo mahususi kabisa kwa ajili ya kupambana na majanga ya moto.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninachotaka kuchangia hapa kweli hoja ni nzuri, lakini siungi mkono hoja kanakwamba kazi hii kubwa ipelekewe halmashauri zetu, badala yake Serikali iongezee nguvu Wizara yetu kupitia Jeshi la Zimamoto ili iweze kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa hilo. Kwa hiyo siungi mkono hoja kwamba halmashauri zetu zipewe jukumu hili kubwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii hoja sijui kama imewekwa kwenye vishikwambi vyenu? Mnayo kwenye vishikwambi? Tuielewe vizuri hoja ya Mbunge, yeye anataka magari yanunuliwe na zile halmashauri zenye uwezo, halafu zifanye siyo kwamba kazi ifanywe na halmashauri, kazi ifanywe na Jeshi la Zimamoto, lakini kwa sababu Jeshi la Zimamoto halina uwezo wa kununua magari kwenye baadhi ya halmashauri, halmashauri zinunue ziipe Jeshi la Polisi. Usiseme hapana, wakati ndiyo hoja iliyoko hapa Mheshimiwa Salome, uko nayo hoja hapo? Uko nayo hoja?

Ehee! Sasa ukisema hapana ni kwamba siyo hoja ya Mbunge? Sasa mimi nilikuwa naeleza kipi na wewe unasema hapana kwenye hoja ipi?

Waheshimiwa Wabunge, haya nadhani tumeelewa sasa hoja ya Mheshimiwa Mbunge ili tunapochangia tujue tunachangia kwenye hoja aliyoileta hapa mbele.

Mheshimiwa Nicodemas Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Deogratius Njau na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyoko mezani kwetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga hoja ya Mheshimiwa Mbunge aliyoileta hapa mbele yetu, naunga mkono kwa sababu haya mambo yalishanitokea mara tatu, siku moja nikiwa kwenye Mkoa wa Singida basi lilipata ajali mbele yetu, pale kuna Mji wa Ikungi ilivyoonekana *fire* mpaka itoke mkoani, lakini pia kwenye Jimbo langu yalishanitokea mara mbili kwenye Mji wa Lulembela.

Mheshimiwa Spika, hakuna umuhimu kama kuwa na gari la zimamoto kwenye mji. Sasa hivi dunia imebadilika, Serikali imepeleka umeme kila mahala, kila vijiji kwenye jimbo langu vimeishapata umeme, lakini huu umeme wakati mwingine huwa unapiga shoti. Utayajua siku shoti ikikutokea ukiwa jimboni na ukapigiwa mwalo na wananchi ukaenda kwenye sehemu ya tukio.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali kwanza inatakiwa ilichukue hili suala kama jinsi inavyochukua kwenye habari zingine za maendeleo. Pamoja na kwamba zipo halmashauri kiukweli zingine hazina uwezo wa kuweza kununua magari, lakini Serikali Kuu ikitoa maelekezo na maagizo kwamba kuhakikisha kila halmashauri iwe na gari la zimamoto ikiweza hata magari mawili, mimi ndiyo maana nasema namuunga mkono Mheshimiwa na ahsante sana Mheshimiwa Tarimo kwa kuleta hii habari kwa sababu mimi yalishanitokea pale mjini Masumbwe na Serikali iweke msisitizo tu, iwaelekeze halmashauri pamoja na Madiwani kushirikiana na Jeshi la Zimamoto ili kuweza kuhakikisha kwamba tunapata magari pamoja na vifaa vya kuzimia moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miji yetu inakuwa kwa kasi, mimi ninazo kata 17 ambazo kila siku wananchi wanapata pesa wanajenga, lakini umeme kila mahala kama nilivyosema umewekwa. Tunavyo viwanda kiasi kwamba ikitokea shoti ya moto, gari itokea Geita kuja Masumbwe umbali wa zaidi ya kilometa 120 utakuta hiyo nyumba imeteketea.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, mimi naomba Serikali kupitia mfumo wake iwasisitize halmashauri kuweza kununua haya magari ya zimamoto, mimi Mbogwe nipo tayari kwa niaba ya wananchi wa Mbogwe kwa sababu tumeishapoteza baadhi ya maeneo watu wanaouza hata mafuta haya ya madumu, inatokea mtu anavuta sigara, nyumba inalipuka unaenda kwa askari hawana vifaa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia upande wa Wizara ya Mambo ya Ndani, hawa askari ni wachache sana. Kwa mfano kwangu nina askari wawili tu, ukiangalia askari wawili wananchi mko zaidi

ya 400,000, nyumba ziko zaidi ya milioni mbili, sasa hawa askari na wenyewe hawatoshi waongezwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi Mheshimiwa Mbunge nakuunga mkono na una akili sana na Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa kuwa na wewe ni Mbunge mwenzetu nina imani hata Mbeya huwa zinatokea hizi ajali, tunaomba utuunge mkono kutoa msukumo kuhakikisha kwamba halmashauri jambo la kwanza kwenye bajeti, watenge bajeti ya kuweza kununua magari na maisha mengine yaweze kuendelea. Tukipeleka haya mambo kimasihara masihara tutakuwa tunapoteza binadamu wenzetu kwa uzembe kabisa ambapo kila halmashuri ina uwezo wa kufanya na pesa nyingi kwa kweli zinaibiwa tu, zinaliwa hovyo hovyo tu hata kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini kungekuwa na umuhimu wa kusisitiza kwamba lazima muwe na gari kwenye wilaya hii, ingekuwa ni nafuu sana na tutaonekana viongozi wenye akili nzuri sana baada ya kuweka misingi imara ya kuweza kuhakikisha kwamba tunaboresha kwenye hii nafasi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu na Mheshimiwa Ally Kassinge ajiandae.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niunge mkono hoja hii, lakini niombe kuwe na marekebisho kidogo kwenye ile hoja ya kwanza kipengele cha kwanza au Azimio la kwanza anasema; "Serikali ilete Muswada wa Sheria Bungeni ili kuweka utaratibu wa

kuwezesha halmashauri kutenga fedha katika bajeti zake kwa ajili ya kununua magari ya zimamoto, vifaa na mambo mengine ya uokoaji." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe kuwe na *option* kwa sababu halmashauri hazifanani, kuna halmashauri huku chini ziko hoi kabisa, kwa hiyo, niombe kuwe na *option* halmashauri zenye uwezo kwa sababu chini huku tunajua kuna halmashauri haziwezi kabisa kufanya haya mambo, kwa sababu gari moja ni zaidi ya shilingi milioni 900 kwa hiyo, inawezekana kabisa kuna halmashauri hazitaweza, lakini naunga mkono hoja yake na mambo mengine yaendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu nishukuru mpaka sasa Jeshi la Zimamoto walipokea magari 12 ya kisasa ya kuzima moto na sisi tulienda kuyazindua. Hizi ni jitihada za Mheshimiwa Rais ambaye ameenda kutafuta fedha na kuleta magari haya. Zimamoto hawapati bajeti ya kutosha, tunaweza tukawapiga mawe, lakini mpaka mwezi wa pili hawakuwa wamepata hata mia. Sasa unawapigaje mawe hawa watu? Serikali ichukue jukumu lake, ipeleke fedha kwa wakati, halafu tuwabane wakiwa wana fedha, hawana kitu halafu tunawabana, tutakuwa tunawaonea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Rais ameweka mkakati wa dola milioni 100 ambazo zitakuja na magari ya kisasa yatanunuliwa. Kama magari 12 tumeyaona hayo mengine yatakuja, lakini tusibweteke kwa sababu hili jukumu siyo la Mheshimiwa Rais. Hili jukumu ni la kwetu kama Wabunge na Bunge likitenga pesa ziende, tunatenga fedha haziendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake halmashauri nyingi huku chini zinapata hizi shida, lakini Wizara ya Maji pia ina wajibu wa *fire hydrants* kule chini hakuna maji. Kuna sehemu nyingine zinapata majanga ya moto, watu wa Zimamoto wakienda hakuna maji. Kwa hiyo, Wizara ya Maji inawajibika, lakini kuna miundombinu, kuna sehemu kabisa kunatokea janga la moto gari haiwezi kufika, ni mpangilio holela. TAMISEMI na Wizara ya Ardhi washirikiane ili kuweka utaratibu mzuri ili hata likitokea janga la

moto gari iweze kufika mahali, huwezi kuwalaumu Zimamoto wakati gari haiwezi kufika ikifika inakwama, wanaangalia nyumba zinateketea, miradi inateketea hawawezi kuruka juu wakafika pale wakaenda kuzima moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *sometimes* tunaweza kuwalaumu na wananchi wanaweza kuwaona kama hawawezi kufanya kazi, lakini hawana namna ya kufanya kwa sababu wanakutana na vikwazo na vikwazo hivi ni vingi, ni lazima Wizara hizi zote zikae kuona namna gani ufanisi unaweza kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Kassinge na Mheshimiwa Tarimba Abbas ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwanza niseme mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Tarimo na naunga mkono kwa sababu hata tukisema kwamba Serikali leo inaleta gari moja kila halmashauri, bado umuhimu wa sisi halmashauri zetu hasa zenye uwezo na ambazo miji inatanuka kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuchukulia mfano wa Mji wa Geita, Mji wa Geita una watu takribani 400,000. Kwa hiyo, hata kama Serikali italeta leo gari la zimamoto ule mji unahitaji zaidi ya gari nne za zimamoto, kwa sababu haiwezekani mkawa na gari moja ambalo yakitokea majanga mawili au likitokea janga likiishiwa maji ikimbie ikazime, irudi ikimbie ikazime. Kwa hiyo, naunga mkono hoja kwa mantiki kwamba jambo hili lifanyike kwenye halmashauri zenye uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niweke kumbukumbu sahihi hapa tusije tuka-*shift burden,* kwa sababu katika mazingira ya kawaida upo uwezekano ukiliingiza ukaleta sheria, ukaliingiza kwenye kulifanya kuwa la lazima kwenye halmashauri, zipo halmashauri makusanyo yake kwa mwaka ni shilingi bilioni mbili. Gari moja la zimamoto ni

shilingi bilioni moja, lakini changamoto kubwa ninayoiona ukiliweka suala hili kuwa la lazima, hizi halmashauri hazina namna ya kukwepa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tusi-*shift* hii *burden*, Serikali iendelee na wajibu wake, kwanza kutambua maeneo ambayo kwa kweli yanahitaji kufanyiwa marekebisho kwa mfano miundombinu. Kwa ujumla miji mingi inajengwa yaani inajengwa tu kama vile jambo hili halijulikani. *Let us take this issue in a holistic and realistic* yaani tuichukue kwa upana wake mkubwa tangu kwenye mipango miji, hao zimamoto wenyewe hawapo, wengine hawana ofisi, ukiwakuta hawana gari yaani changamoto ni nyingi kuliko gari la zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali isikwepe huu mzigo, iendelee kushughulika nalo, lakini halmashauri zenye uwezo tuangalie namna tunavyoweza kununua vifaa na kuwakabidhi ili waweze kushughulika nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuunga mkono na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Tarimba na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda ajiandae.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Jacob Tarimo kuhusiana na hoja iliyopo mezani ya halmashauri zetu hasa za miji, majiji na manispaa kuingia *MoU* na Jeshi la Zimamoto kwa lengo la kushirikiana katika utatuzi wa majanga pamoja na mioto ambayo mara kwa mara imekuwa ikitokea katika miji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge, moto hauna wingi… *(Kicheko)*

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nirekebishe kwamba *MoU* ambayo itaingiwa na miji yetu,

manispaa na majiji kwa upande mmoja na Jeshi la Zimamoto kwa upande mwingine kwa lengo sasa la kushirikiana katika kutatua majanga pamoja na moto ambao umekuwa ukitokea mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kuunga mkono hoja hii na naunga mkono hoja hii nikiweka msisitizo kwamba moto na majanga ni sehemu ya vitishio vya usalama katika maeneo yetu, lakini jukumu la ulinzi na usalama Kikatiba, Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa zimepewa jukumu hilo la ulinzi na usalama na kwa maana hiyo Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa ikiwemo miji, majiji na manispaa kwa namna yoyote ile iwayo huwezi ukazitenganisha na jukumu la msingi la ulinzi na usalama wa watu katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ni kwamba Jeshi letu la Zimamoto limekuwa likipata changamoto ya miundombinu isiyoridhisha pale ambapo majanga ya moto yamekuwa yakitokea, lakini jukumu la upangaji miji kisheria ni jukumu la miji yetu, manispaa zetu na majiji yetu na kwa maana hiyo huwezi ukazitenganisha Mamlaka za Serikali za Mitaa na Jeshi la Zimamoto katika maeneo ya kupanga miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa changamoto ambazo zimebainishwa na baadhi ya wachangiaji ni upungufu au kutokuwepo kwa kabisa kwa *fire hydrants* katika miji yetu, lakini ni nani atakayeainisha maeneo haya ya *fire hydrants*? Ni jukumu la pamoja sasa kati ya halmashauri zetu pamoja na Jeshi la Zimamoto kutenga maeneo ya *fire hydrants* ili Jeshi la Zimamoto liweze kupata wepesi pale majanga yanapotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na baadhi ya wachangiaji kwamba halmashauri zetu hazifanani kimapato, lakini niweke wazi hapa kwamba *MoU* ambayo itaingiwa haitailazimisha kila halmashauri zichukue hili jukumu la kusaidiana Jeshi la Zimamoto, itategemea uwezo wa halmashauri husika, lakini pia itategemea halmashauri inadhani ishirikiane na Jeshi la Zimamtoto katika eneo la hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme kwamba kumekuwa na *misconception* kidogo kuhusiana na mapato ya halmashauri ikidhaniwa kwamba bajeti za halmashauri zinakusudiwa zile tu ambazo ni kwa ajili ya mapato ya ndani *persée,* hapana. Halmashauri ambazo zitaingia *MoU* na jeshi hili kwa kununua vifaa au magari zitakuwa na *avenues* mbalimbali za kutafuta vyanzo vya mapato ikiwemo *grants* kutoka kwa wahisani mbalimbali na kwa maana hiyo tusipate hofu ya kudhani kwamba halmashauri tutakuja kuzibebesha mzigo kwa kusaidiana na Jeshi la Zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mheshimiwa Michael Mwakamo ajiadae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Tarimo kwa kufanya kazi ya kubuni kuleta hoja hii, ahsante kwa kufanya kazi ya Kibunge na hiyo ndio kazi ya Kibunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze Mheshimiwa Kassinge umenifilisi, lakini mimi nina nyama zaidi ya hizo ambazo umezitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi ukaiepuka halmashauri yoyote ile ya mji kwa sababu halmashauri ni *planning authority* kwa mujibu wa sheria. Wao ndio wanaopanga mji, barabara na njia za maji. Wao wanaweka hata maeneo *fire hydrants* inapotakiwa iwe, unaiepuka vipi halmashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si lazima halmashauri itoe fedha, kinachohitajika hapa ni kuhusishwa kwa halmashauri katika taratibu nzima za upangaji wa miji. Najua Mheshimiwa Rais ametupatia magari mengi sana ya zimamoto, hata Dar es Salaam

ametupatia, lakini hebu iangalie ilivyo, kwa mfano mzuri nawapatia mifano mitatu tu. Magomeni Mapipa pametokea moto ambapo siyo mbali hata kilometa moja na kilipo Kituo Zimamoto, bado hawakuweza kutusaidia, nyumba ziliungua zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kule Soko la Mchikichini hali kadhalika hawako mbali na Kituo cha Zimamoto. Ukaenda Soko la Kariakoo hawako mbali na vituo vya zimamoto. Pia Dar es Salaam barabara zipo finyu, msongamano wa magari ni mkubwa, lakini hata magari ya zimamoto yakifika katika eneo la ajari *fire hydrants* hazifanyi kazi. Wanafanyaje kazi ya kuweza kusaidia kuzima moto?

Mheshimiwa Spika, niwape takwimu tarahe 15 Mei nilivyokuwa nachangia kwenye bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani nilizungumzia masula ya zimamoto peke yake na katika mambo yale niliwakumbusha utafiti uliofanywa mwaka 2013 kwamba utafiti ule unaonesha *fire hydrants* katika Jiji la Dar es Salaam zilikuwa 2,600 na 1,268 hazifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zilizokuwa zikifanya kazi mwala 2013 ni 74 tu, sasa hivi zinazofanya kazi ni 108. Taratibu za uwekaji wa *fire hydrants* ni futi 500 na zisizidi futi 800, hizo hazipo.

Mheshimiwa Spika, sasa hata kama ukiwa na magari ya kutosha, gari zikienda pale zikazima moto na wanapozima moto maji yamemalizika inabidi waondoke wakatafute maji, yaani unataka kuniambia moto umekaa pale unawasubiri *fire* waje pale walete maji? Hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana *fire* wakimaliza kuzima, wamezima moto tu, lakini uokoaji haupo. Mali zinateketea, hivyo ili kuweza kuisaidia *fire* mimi naunga mkono hoja nzima ya Mheshimiwa Tarimo kwa sababu kama nilivyosema *planning authorities* lazima zihusike, watu wa maji lazima wahusike, *fire hydrants* ni kitu muhimu sana na umuhimu wake ni kwamba hata maji yanapokuwa na *pressure* ukifunga lile bomba la kuzimia moto hata gari huhitaji. Wakati mwingine maji yale yanaweza

kutumika kuweza kuzimia moto. Kwa hali hiyo mimi nimelitaja tu hilo eneo la *fire hydrants,* lakini ni dhahiri kabisa hoja hii ni muhimu na Serikali iichukue, ifanyie kazi ili kuweza kuokoa watu wetu, miji na mali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mheshimiwa Vincent Mbogo ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweka mchango wangu kwenye hoja ya ndugu yetu Mheshimiwa Tarimo ambayo ni hoja nzuri na muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwamba ni nzuri na sisi wote tunakiri kabisa kwamba tunalo Jeshi la Zimamoto na uokoaji lenye wajibu huo ambalo lipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini kwa kweli halina vifaa vya kutosha na hata watendakazi Askari wa Zimamoto na Uokoaji si wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nilitaka niseme kwamba kwa hali ya sasa ya maendeleo hatutaweza kuwa na magari ya zimamoto ya kutosha, hatutaweza kwa hali ya sasa kuwa na vifaa vya kutosha vya uokoaji, ni lazima tujielekeze zaidi katika kuelimisha umma wetu katika baadhi ya maeneo juu ya namna nzuri zaidi ya kujiokoa na kuchukua tahadhari. Magari ya zimamoto na vifaa vya ukokoaji viwepo, lakini tukisema kwamba vya kutosha sehemu fulani yawe magari kumi au 15, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninachotaka kusema ni kimoja tu, naungana na wanaosema kwamba kuwabebesha halmashauri kuwa hili ni sehemu ya wajibu wao siungi mkono hiyo hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe unafahamu halmashauri imepewa majukumu ya kutoa taka katika maeneo yetu, magari ya kusomba taka hawajaweza kukidhi, hayajaweza kutosheleza, bado kuna malalamiko ya kurundikana kwa taka katika maeneo ya masoko na maeneo mengine chungu mzima. Pia siyo hilo tu, maboma ya zahanati na shule wanashindwa kuyamalizia mpaka wanakuja kuomba hapa Serikali Kuu isaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninachoweza kusema ni kwamba hoja ni nzuri na zaidi tujielekeze kutazama pande zote mbili. Wengi wanazungumza hapa suala la kuzima moto na wengine wanazungumza uokoaji wanafikiri maana yake ni kuokoa mali, ni kuokoa watu na hii ina maana kwamba watu wanaopata matatizo kwenye Ziwa Tanganyika, maziwa mengine na baharini na wengine wanaopata majanga ya mafuriko wanaopata milima ku-*slide* waweze kuapata nafasi ya kuokolewa.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**TAARIFA**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nataka tu nimuongezee Mheshimiwa Kilumbe kwamba, thamani ya gari la zimamoto moja kununua ni kati ya shilingi milioni 800 mpaka shilingi bilioni moja peke yake. Hiyo ni manunuzi tu hujaweka *service* na matumizi mengine, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa…

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa unasubiri uitwe tena. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda unaipokea Taarifa hiyo? *(Kicheko)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, napokea Taarifa. Unajua nilikuwa nakimbizana na muda, niwie radhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema hiyo bei iliyotajwa ya gari ya zimamoto kwa gari ya taka ni kama shilingi milioni 100 tu nazo zinawashinda halmashauri nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka niseme hoja ni nzuri, lakini tujielekeze katika harakati ambazo Mheshimiwa Rais wetu ameanza kuzionesha kama hivi amepata fedha aongeze vifaa na sisi tuwe tunaitazama mara kwa mara bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani hasa katika watu wa zimamoto na uokoaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kwa upande wangu ni kweli kabisa kwamba halmashauri na hasa watu wa Mipango Miji hizi *fire hydrants* nyingi zimejengewa majengo, badala ya maeneo haya ya *fire hydrants* kuwa wazi ili watu waweze kuchukua maji wakati wa kuzima moto, kuna majengio yamejengwa hapo hii miundombinu tena imekuwa haipo.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hilo tuwafundishe na kuwasaidia watu wetu suala la kununua na kuweka katika majumba yako kitu kinaitwa *fire detector* ili iweze kuonesha ni wakati gani moto unataka kutokea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, makofi yanapigwa anayeunga mkono hoja, makofi yanapigwa aliye kinyume, sasa na wapigaji makofi ni wale wale. Sasa hapo ndio sijaelewa kama wengi wanaunga mkono hoja au hapana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Michael Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mtemvu kisha nilimtaja Mheshimiwa Aida Khenani au Vincent Mbogo?

Sawa hawa wanatoka Jimbo moja, kwa hiyo sawa. Mheshimiwa Mwakamo Michael atafuatiwa na Mheshimiwa Vincent Mbogo, kisha Mheshimiwa Mtemvu Issa ajiandae.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi maana wakati unaorodhesha kulikuwa na namna ya kuona watu wa Pwani na Dar es Saalam ni wengi, lakini nashukuru umenipa nafasi na nimepata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwa dhati ya moyo nimpe pia shukrani na pongezi sana Mheshimiwa Tarimo kwa kuleta wazo hili mezani japo wazo linalohitaji tafakari ya kutosha. Kwa namna alivyolileta na Mheshimiwa Spika navyosimamia utaratibu unaona kama inakulazimisha uunge mkono hoja kwa kila jambo ulilolisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ukiangalia katika hoja uliyoiwasilisha ni hoja ya msingi, lakini lile jambo unalolitamka juu ya masuala ya ununuzi wa magari pekee kama sehemu inayotakiwa liende halmashauri ndilo linaloleta tabu kwenye kujadili kutokana na uwezo wa hizo halmashauri husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa suala la zimamoto ni suala ambalo lina changamoto kubwa kwenye majimbo yote nchini na hii ni kutokana na utendaji wake unaosababishwa na uwepo wa changamoto za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nimesimama kwa kuja na fikra na mawazo ya kuchangia katika hoja hii kwa namna ambavyo nafikiri tunaweza tukawa ni sehemu ya kutatua tatizo tulilonalo.

Mheshimiwa Spika, ukirudi kwenye sheria zilizounda Serikali za Mitaa tunatumia Sheria Namba 7 na 8 ambazo ndizo zimeanzisha Serikali zetu za Mitaa. Muundo wake ukiunagalia moja ya jukumu la msingi la hizi Serikali za Mitaa ni kutoa huduma kwa wananchi, ndio jukumu kubwa na ukiangalia majukumu yote ambayo yanafanywa na zimamoto unayaona ni kama sehemu ya kutoa huduma kwa sababu yanakimbilia pale sehemu ambapo kuna majanga na kuliondoa hilo janga kwa wakati husika na baada ya kuliondoa hakuna chochote ambacho mwananchi aliyeondolewa janga hilo anapaswa kufanya mchango wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu hiyo basi unaona msingi wa shughuli za zimamoto kwenda kuungana na shughuli za halmashauri kwenye mipango yake, kwa sababu ni kazi ambayo halmashauri wanatakiwa waifanye kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Kwa mfano, halmashauri zote ndiyo zinazoandaa mipango kwa ajili ya ujenzi wa shule na zahanati na hii yote ni kwa sababu ya kumlinda mwananchi huyu ili asiingie kwenye majanga mbalimbali, lakini ukiangalia Zimamoto wanafanya shughuli zao zinazokwenda kuokoa majanga hayo hayo ya jamii, lakini jina pekee lilivyokaa kwanza tayari linaleta ukakasi.

Mheshimiwa Spika, ninazungumza masuala ya zimamoto, lakini kazi inayoenda kufanywa kule ni kubwa sana. Kwa hiyo, tuna kila sababu Serikali kukaa chini na kutafakari kwa kina na kuboresha namna ya utendaji kazi zake ili tuziunganishe sehemu ya majukumu ya zimamoto wawe na mahusiano makubwa na halmashauri za nchi hii katika mambo mbalimbali ya mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hata ukiangalia sisi kama halmashuri ndio tunakaa chini kuangalia eneo gani liwekwe viwanda. Hebu tujiulize kwenye maeneo ambayo tunawekeza viwanda, kuna utaratibu gani wa kuandaa miundombinu ya kukabiliana na masuala ya majanga? Tunakabiliana nayo kwa namna gani? Tuna miradi ya maji mingi tunaiendesha kwenye halmashauri zetu. Ni namna gani miradi ya maji inatengeneza miundombinu ya kwamba ikitokea majanga ya moto haya magari yawe yanapata maji kwa njia ya ukaribu?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi niombe kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Tarimo kwa namna alivyoileta, lakini naona ametufungulia mlango wa kuendelea kutafakari, tupate wasaha wa kutosha kuona ni namna gani tunaweza tukaondoa hizi changamoto kwenye jeshi letu kwa sababu Jeshi la Zimamoto lina changamoto nyingi za kutosha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba sana na nashauri kwamba pamoja na kuona kwamba Zimamoto wanatakiwa wajitegemee, lakini ikiwezekana utendaji wao wa kazi ushushwe sasa kutoka kwenye ngazi za wilaya uwekwe katika kila ngazi ya

halmashauri ili mahusiano ya mipango yao ifanywe ndani ya mabaraza ili tuone yapi yanaweza kufanywa ndani ya halmashauri na yapi yanaweza kufanywa na Serikali Kuu, hatimaye mwisho wa yote tuwe tumemaliza changamoto za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vincent Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani ajiandae.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Tarimo ya kuhusu Jeshi la Zimamoto na kwanza naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu fikra wanawaza zimamoto ni moto tu, hao ni mjini. Kutokana na maendeleo ambayo sasa hivi Mheshimiwa Rais anatupatia, anajenga ofisi za kisasa na miji inakua, kuna miradi mbalimbali ya kisasa. Zimamoto sasa hivi inatakiwa ianzishe Kitengo cha Zimamoto Jamii kwa sababu askari ni wachache, elimu vijijini hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majanga siyo moto tu, vijijini huku kuna majanga mengi sana hasa wakati wa masika, watoto wanaangukia kwenye mafuriko, visima na mitaro, lakini wananchi hawana elimu na haya majanga hayatangazwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi kuna mkakati wa Wizara ya TAMISEMI kusaidia Wizara ya Mambo ya Ndani kujenga vituo vya polisi, kila kwenye Kituo cha Polisi pawepo na Ofisi ya Zimamoto, ili wananchi waweze kupata elimu ya kuweza kujiokoa katika majanga mablimbali. Majanga mengi yanatokea vijijini, lakini hakuna elimu ya namna ya kuokoa. Kwa hiyo, kuna vifo vingi sana vinatokea vijiji ambavyo siyo moto. Kwa hiyo, hii elimu ya zimamoto ishuke katika kila Kituo cha Polisi cha Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kilumbe ameongelea kwenye Ziwa Tanganyika na maziwa mengine, huko kote hakuna mkakati maalumu wa kujenga ofisi za uokoaji. Boti nyingi zinazama, vituo vya polisi havina eneo la ujenzi wa ofisi za zimamoto. Kwa hiyo, naomba Wizara hii pamoja na TAMISEMI ijengwe ofisi za zimamoto kwa kila kata ili elimu itolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo majanga ya asili na ambayo siyo ya asili, hata kwenye *lift* maeneo mengi yanahitaji zimamoto. Kwa hiyo, Jeshi la Zimamoto ndio tumehuisha kwenye Kamati ndio sasa hivi inakuwa na uwezo wa kupatiwa fedha, mwanzo lilikuwa halipatiwi fedha. Kwa hiyo, kwa sasa hivi ndio limeanza kupatiwa fedha.

Kwa hiyo halmashauri kushirikiana na Jeshi la Zimamoto siyo lazima fedha na halmashauri ambazo hazina uwezo kushiriki tu ili kuliwezesha kuwa na mpango wa pamoja wa namna ya uokoaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Mtemvu atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa Jumanne Sagini ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu juu ya hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Tarimo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Tarimo kwa hoja hii ambayo binafsi imenisumbua kwa muda mrefu sana, hata nilivyoingia asubuhi nikamuwahi kumwambia hongera sana na nitapata bahati ya mimi kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nikushukuru wewe kwa kuniona nje ya utaratibu na mwongozo wa kikanuni, lakini ukatupa nafasi kama alivyosema Mheshimiwa Michael Mwakamo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niseme tu tafsiri ya kwanza ya Jeshi letu la Zimamoto, kwenye taarifa amejaribu kuisema kwamba kabla ya mwaka 2007 tulikuwa tuna taratibu hizi ndani ya halmashauri zetu, lakini Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaundwa kufanya kazi chini ya Sheria Namba 14 ya mwaka 2007 *(Fire and Rescue Force Act)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi sana lazima tuyafahamu, moja, ni kuzima moto na kuokoa maisha na mali katika majanga yatokanayo na moto, mafuriko, tetemeko la ardhi, ajali za barabarani pamoja na majanga mengineyo.

Mheshimiwa Spika, sasa katika upana huu wote hatuoni jeshi hili likiwa na majukumu yote manne haya kama niliyoyasema. Tukiangalia haraka na maono ya wananchi dhidi ya jeshi lenyewe unaweza ukamuona yupo tu kwenye eneo la kuzima moto, lakini humwoni kwenye mafuriko, majanga ya barabarani na majanga mengine ambayo nimejaribu kuyasema hapa kama vile matetemeko ya ardhi na kadhalika. Kule Kagera yalitokea, lakini na maeneo ya hapa Dodoma hatukuwahi kuwaona.

Mheshimiwa Spika, niseme naunga hoja mkono katika mapana ya kwamba pawepo na *MoU* kati ya halmashauri na Jeshi la Zimamoto. Pia na mimi hapa niwe *very specific* ishuke chini, lakini katika zile halmashauri za miji na majiji zenye uwezo zikaisaidie bajeti ya zimamoto kwa sababu kwa Serikali Kuu peke yake kwa majukumu haya niliyoyasema yote kwa majukumu haya kwa mujibu wa sheri inayounda zimamoto, haiwezi kuutekeleza. Kwa hiyo, wakisaidiwa inawezekana wakaweza kufanikisha lakini wale wasio…

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, muda wenyewe jamani.

**SPIKA:** Mtajuana na ninyi huko ni majirani. Kwa hiyo, mtajuana baadaye. Mheshimiwa Mtemvu kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Neema Mwandabila. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ninataka nimwambie kwamba yeye anatoka halmashauri ya mjini Dar es Salaam, haya mambo ya ununuzi wa haya magari ya *fire* inawezekana. Kama halmashauri ya Mji wa Tunduma imeweza kununua, wenyewe Dar es Salaam wanashindwa kitu gani? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu, Taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, hajanielewa tu hoja yangu, ninaona kaunga mkono tu ambacho nilikuwa nakisema, sikukataa kwamba halmashauri za miji na majiji makubwa ziweze kusaidia bajeti kuu ya Serikali kununua ili hawa wadogo wasinunue na ndicho alichokuwa ananiambia nyie mnaweza. Ni kweli tunaweza katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, niweze kukwambia kwa haraka tu, katika majanga haya kama majukumu ya jeshi hili limeshindwa kutokana na vifaa, mimi ninatoa mfano tu mafuriko. Katika kipindi hiki cha mafuriko ndani ya jimbo langu nimepoteza watoto wawili, lakini jinsi gani ambavyo nilikuwa ninajaribu kushirikiana na jeshi hili, lilikuja tu na maji na magari yake, lakini jambo lenyewe ni mafuriko, hawakuja na vifaa vingine.

Mheshimiwa Spika, siku tatu wananchi wa pale wa jimbo lile tulikaa kwenye maji tunatafuta katika njia zetu za *local,* lakini na wenyewe wakaja wakatuunga mkono kwenye kutembea na fimbo. Tukawauliza je, mngekuwa na mbwa si angenusa kwenye vichaka vilivyojifunika?

Mheshimiwa Spika, huwezi amini, ndani ya muda mdogo baada ya siku kumi akapatikana yule mtoto ndani ya kichaka ambacho hakipo hata zaidi ya meta 200. Kwa hiyo, wangekuwa na mbwa ingetusaidia.

**SPIKA:** Haya, ngoja twende vizuri. Mheshimiwa muda wako umeisha lakini unayo hii hoja ya Mheshimiwa Mbunge?

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, ninayo hoja hii.

**SPIKA:** Uko nayo?

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Kifungu (b) yake umeisoma inasomeka namna gani? Muda wako ulikuwa umeisha. Kwa hiyo, huu unaotumia ni wa kwangu. Fungua tu, halafu soma (b) yake anasema nini. Au ni kusomee? Au umepapata?

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nisaidie, ninaona hitimisho. Juu ya hitimisho (b) ... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, haya, (b) yake inasomeka hivi na anasema; "Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria utakaoweka utaratibu wa kuwezesha halmashauri za miji na wilaya kuingia makubaliano ya ushirikiano *(MoU)* na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya kununua magari ya zimamoto na vifaa vya uokoaji. *(Makofi)*

Haya, ahsante sana, ni hapo nilitaka nikusomee.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na kwa hiyo, ninaiunga hoja mkono ya Mheshimiwa Tarimo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante, ahsante sana.

Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Sagini.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu na mimi ninampongeza sana Mheshimiwa Tarimo kwa jambo hili muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia jambo lenyewe linazungumzia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Kwa hiyo, ni jeshi, lakini inahusika

zimamoto na uokoaji. Siyo uokoaji tu kwa sababu moto umetokea, ina maana ni uokoaji kwenye majanga yote.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninajiuliza, wajibu wetu kama Wabunge ni kutenga bajeti na kupitisha na wajibu wa Serikali ni kutekeleza sasa, kupeleka fedha na kutekeleza yale ambayo Bunge limepitisha. Pamoja na jambo jema ambalo amekuja nalo Mheshimiwa Mbunge na ushauri ambao ameutoa, bado ninakubaliana na hoja yake isipokuwa kama ambavyo Wabunge wengine wamezungumza, halmashauri zetu zinatofautiana isipokuwa kama kwa sasa sheria tuliyonayo tu haijazuia halmashauri yenye uwezo kuweza kununua magari na kusaidia zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninajiuliza, hivi kama hili ni jeshi na changamoto zote ambazo tunakutana nazo kama Taifa, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa jambo hili kupeleka fedha? Leo tunapozungumzia halmashauri, halmashauri inahusika na upangaji wa miji, ni wajibu wao. Kwa sababu hata kama zimamoto watapewa fedha kiasi gani, kama mipango yetu ya kupanga miji itakuwa hovyo hawatafanya chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna haki bila wajibu, ili zimamoto walaumiwe ni lazima askari hao wawepo, wawepo na vitendea kazi, lakini Serikali iwape fedha. Wakati ninaendelea kujiuliza maswali nikasema...

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, kuna Taarifa. Inatokea wapi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, inatokea hapa.

**SPIKA:** Ahaa, Mheshimiwa Hamad Chande.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninapenda nimpe Taarifa dada yangu, anachangia vizuri sana, lakini tayari Serikali imeshatoa fedha *USD* milioni 100 mwezi uliopita na wapo katika mchakato wa manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tena Serikali imeenda mbali sana, siyo vifaa vya magari tu. Helikopta zitanunuliwa na boti za zimamoto zitanunuliwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Naibu Waziri ninakuheshimu sana, kwa sababu unasema bado hamjapeleka, kwa hiyo ninakubaliana mpeleke sasa kwa sababu ni wajibu wenu kupeleka hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninataka nizungumze jambo moja.

**SPIKA:** Amesema wameshapeleka.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, wako kwenye manunuzi, hazijakwenda bado.

**SPIKA:** Yeye amesema wameshapeleka, ndiyo neno alilotumia. *(Makofi)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, haya sawa, wamepeleka ya magari mangapi na mahitaji ya nchi hii ni kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ninaweza nikashauri ni kama jambo hili ni kipaumbele chetu tupunguze baadhi ya matumizi ambayo hayana ulazima.

Mheshimiwa Spika, tulipitisha hapa kununua magari ya ma-*DC* zaidi ya shilingi milioni 400. Kama kipaumbele chetu ni magari ya zimamoto, kulikuwa na sababu gani ya kupeleka hizi fedha zote kwenye magari ya ma-*DC*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, magari ya ma-*DC* wanaweza wakatumia hata magari yaliyopo kwenye halmashauri; zimamoto inahitajika kila siku. Kwa hiyo, lazima tuwe na kipaumbele kama Serikali na hata kama tunasema tumepeleka, mimi ninaamini hata nusu... *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo wafanyabiashara wanalipa hizi fedha kila mwaka kwa ajili ya zimamoto. Sasa wanapolipa zinakwenda wapi? Kwa nini zisiende kufanya hizo kazi. Kwa hiyo na wao wenyewe wafanyabiashara na nikwambie; mimi nimekaa nao Ijumaa wafanyabiashara wa kwenye jimbo langu. Wanasema hatutalipa kuanzia leo, hatujawahi kuliona gari la zimamoto hata siku moja lakini wakija hapa wanatukaba tunalipa fedha. Tunalipa fedha za nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali, tusipeleke huu mzigo kwa halmashauri, ni wajibu wa Serikali Kuu, tutimize wajibu wetu. Hili jeshi tunalihitaji, lina kazi muhimu, liwasaidie Watanzania. Halmashauri ambazo zina uwezo zifanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kusisitiza na kumpongeza Mbunge kwa jambo hili muhimu sana, lakini tuwe na kipaumbele tupunguze matumizi ambayo hayana ulazima kwa Taifa letu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jumanne Sagini, mtoa hoja ajiandae kuhitimisha hoja yake.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na Wajumbe waliozungumza kwa dhamira ya kuimarisha huduma za zimamoto na uokoaji katika nchi yetu, lakini nichelee tu kukubaliana na hoja hizi kama zilivyotolewa zote na kama lengo lake ni kwenda kufanya marekebisho kuanzia mwaka ujao wa fedha wa kile kinachoendelea wa kile kinachoendelea au kilichokwisharidhiwa na Bunge lako kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tayari tumeshapitisha bajeti za TAMISEMI zikiwemo mikoa na halmashauri na sidhani kama tulikuja na mtazamo huu ambao tunataka *resources* zilizopo kwa

ajili ya kutekeleza majukumu ya msingi ya Serikali za Mitaa yaliyoko sasa zihamishwe ziende kugharamia majukumu ya zimamoto na uokoaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba kwa miaka mingi eneo hili la zimamoto na uokoaji lilikuwa halijawekezwa vya kutosha, lilikuwa halijaimarishwa, lakini Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika miaka mitatu iliyopita ameonesha dhamira na utendaji. Kwanza kwa kuwaongezea nguvu kazi, zaidi ya watumishi 800 wameajiriwa kama askari wa zimamoto na uokoaji, lakini nikiri pia nilikuwa kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi miezi michache iliyopita, mafunzo yenyewe ya uokoaji yalijikita zaidi kwenye kuzima moto. Uokoaji wa baharini, ziwani ilikuwa ni changamoto. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, lakini...

**SPIKA:** Mheshimiwa Jumanne Sagini, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ninataka kumpa taarifa mzungumzaji, hili jambo ni pana sana.

Mheshimiwa Spika, mimi ninadhani aliyeleta hoja hii ametukumbusha kwamba suala la majanga ni kubwa sana katika nchi yetu kwenye halmashauri zetu. Kwa hiyo, amekuja kutupatia mawazo kwamba tuteremke mpaka chini huko ndani. Halmashauri zetu ziungane na Idara ya Zimamoto zisaidie namna ya kuokoa wananchi kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukilizungumza kama kupata chanzo cha mapato hatutaweza kuliokoa hili jambo. Tuongee kama kwamba halmashauri ziungane na upande huu wa zimamoto, kwa maana

hata kabla ya mikataba hiyo kuwepo na mawazo ya kuzuia majanga badala ya kufikiria zaidi kwenye hela. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jumanne Sagini, unapokea Taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninatafuta ipi niipokee, lakini ninashukuru. Ni kweli lengo ni kuimarisha kama Mheshimiwa Mbunge mmoja alivyozungumza.

Mheshimiwa Spika, kwa *infrastructure* iliyopo sasa hivi ya kisheria na kisera, hakuna kikwazo chochote cha zimamoto kushirikiana na halmashauri na wamekuwa wakifanya mambo mengi kushirikiana na Serikali Kuu.

Kwa hiyo, ambacho ninataka kushauri wakati ninazungumza nini kimefanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, ni pamoja na kuwaingiza vijana wetu hawa wa *fire* na uokoaji kuingia ushirikiano na timu kama hii Zanzibar kwa KMKM kwa ajili ya uzamiaji na mambo yanayotokea kwenye majanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa lingine amelisema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, mwaka huu tayari wamepewa fedha za kuwezesha kununua magari yatakayopelekwa kwenye taasisi 150 zikiwemo halmashauri zetu zote na mikoa yote na lengo ni kuimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; sipingani kabisa na dhana ya kuimarisha uhusiano kati ya zimamoto na uokoaji.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa inatoka wapi?

Mheshimiwa Jumanne Sagini kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Reuben Kwagilwa.

**TAARIFA**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa niliyokuwa ninataka kumpa mzungumzaji ni kwamba wakati akiongelea habari ya fedha zilizotengwa mwaka huu ninamkumbusha kwamba mwaka 2023/2024 tulitenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kununua magari matano na magari hayo hayajanunuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye magari hayo ulikuwepo mgao wa gari kwenda Handeni ambako ndiyo kuna Msomera, Mradi wa Kitaifa ambapo tumewapokea wenzetu kutoka kule Ngorongoro, lakini si tu hivyo mahali ambapo tuna *highway* kubwa ambayo kila siku magari yanayobeba gesi yanaungua na kuteketeza watu pale. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshakugongea.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ukiachia mbali matukio matukio ambayo yamekuwa yakitokea kwenye mji wa Handeni kama kuunguliwa nyumba kwa Mzee Ally Mhandeni, Mzee wangu Asenga na Mzee Mwingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana ninashukuru.

**SPIKA:** Haya muda wa kuchangia Mheshimiwa Mbunge umeisha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Sagini, muda wako amemalizia Mheshimiwa Mbunge. Haya ninakupa dakika mbili malizia. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninataka kushauri kwamba jambo lenyewe kama lilivyozungumzwa tunaona ni *multisectoral*, ni suala mtambuka. Limegusa Wizara ya Maji, limegusa Wizara ya Ardhi kwenye mipango miji, limegusa TAMISEMI, limegusa Mambo ya Ndani ya Nchi yenyewe, Ofisi ya Rais kwenye miundo na taasisi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, ungetoa nafasi Serikali ilichukue jambo hili ili lichambuliwe na wadau wote hawa ili tunapolizungumza kama Wabunge wengi walivyosema, tulizungumze *comprehensively* kwa upana wake kuliko kuangalia maeneo ya uwezeshaji wa vitendea kazi tu, kwa sababu hata elimu inatakiwa ili watu wetu wawe na utayari na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, uje uhitimishe hoja yako. *(Makofi)*

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa namna ambavyo umeendelea kuusimamia mjadala huu na mimi ninachukua nafasi hii kuwashukuru wale wote waliochangia na wote waliochangia wameendelea kuboresha hoja hii na kutuwekea mazingira mazuri ya namna ya kuwahudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitagusia baadhi ya maeneo, hakuna ubishi kwamba tunahitaji *manpower* eneo hili, hilo halina ubishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la zimamoto na uokoaji, baadhi ya watu wamekimbilia kwenye moto tu, lakini mtoto akitumbukia kwenye shimo la choo kunahitajika utaalamu wa kumtoa. Kwa hiyo, ndiyo maana ninasema kuna vitu vingi vya kufanya kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo maana mimi kuna hoja zinazokuja, kwa mfano ile Tume ya Haki Jinai inataka kurudishwa kwenye halmashauri, mimi hilo siliungi mkono kwa sababu badi ninajua halmashauri nyingi hazina uwezo wa kulisimamia hilo.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba halmashauri tu hazina uwezo, hii shughuli ya uokoaji ni shughuli inayohitaji amri za kijeshi, kutumia amri za kiraia moto unawake watu waende siyo rahisi.

Kwa hiyo, kuna baadhi ya vitu vilivyoko kwenye Haki Jinai, mimi sitaki hata kuvigusa. Kwa hiyo, ndiyo maana bado ninasisitiza jeshi libaki kuwa jeshi na hii kazi ifanyike kijeshi, lakini halmashauri tusiondolewe wajibu wetu au namna ya kushiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru mchangiaji mmoja amesema hawajazuiwa lakini ninajua kabisa, sisi Moshi Mjini tulikuwa na magari tuliyopewa na miji dada (miji marafiki), lakini lilipokuwa jeshi tuliwapa na jeshi waliamua iende wapi.

Mheshimiwa Spika, mimi kwenye hoja yangu ninamaanisha, kama Moshi Mjini tukishirikiana na ninyi kununua gari au tumepewa na wadau, libaki pale kwa matumizi yetu, jeshi mwendelee kulisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri, hata pale Moshi Mjini kabla ya gari mpya ambayo tumeipata, gari iliyokuwepo ilikuwa inahitaji *service,* jeshi halikuwa na hela na halmashauri hawana kifungu cha kwenda kutengeneza gari la Jeshi la Zimamoto. Kwa hiyo, ndiyo maana ninasema kuwe na ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwakumbushe, ushirikiano huu hautakuwa mpya, viwanja vya ndege viliingia makubaliano na jeshi, vyenyewe vinanunua yale magari vinayasimamia, vina-*service* lakini wanaoyafanyia kazi ni Jeshi la Zimamoto. Kwa hiyo, nilikuwa ninasema hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo ninahitaji ufafanuzi, sikusema iwe lazima kwa sababu siyo kila mahali kuna maghorofa. Ninasema kwa halmashauri zenye uwezo na kuna uhitaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Moshi Mjini tumeunguliwa Soko la Mbuyuni, ndani ya mwaka mmoja tumeunguliwa mara mbili. Mara ya kwanza tulilizima likiwa nusu, mara ya pili liliisha lote. Sasa shida iko wapi? Wale wafanyabiashara wadogo hawana *insurance*. Mtaji wake ukiungua pale na vitu vyake maana yake ndiyo ameanza *zero, zero* kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale ni wananchi wetu tunahitaji kuwahudumia na ndiyo maana nikasema halmashauri zenye uwezo na kwa nini nimesema kwenye uwezo, gari itakayohitajika Dodoma kwa jinsi ya majengo yaliyoko Dodoma, siyo sawa na Dar es Salaam. Sisi tunaweza tukanunua ya kufanana nchi nzima, lakini Dar es Salaam wana majengo ya ghorofa 36. Gari yao itahitajika ambayo labda ina *lift* zaidi na uwezo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, halmashauri ikiona ina sababu ya kuwekeza pale kuokoa maisha na uhai wa wananchi wake, basi iweze kufanya hivyo, lakini kuna maeneo kwa mfano, ninakubaliana kabisa na mawazo yaliyoletwa ya kusema kwamba hili suala linahusisha Wizara nyingi, kwa hiyo ni suala mtambuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli, Wizara ya Ardhi, TAMISEMI, Wizara ya Maji, lazima zikae pamoja katika kupanga kwenye kushughulikia hili jambo. Hilo mimi ninakubaliana nalo 100% kwa sababu *fire hydrant* nyingi zimefukiwa na barabara na barabara zinajengwa *either* na *TARURA* au na *TANROADS,* lakini *fire hydrant* ni za Wizara ya Maji na Mamlaka za Maji. Ni lazima wakae pamoja ili kuweza kufanya hayo mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna haja pia ya kuangalia namna ya kuweka ulazima. Kwa mfano, kila mtu anafikiria gari ya *fire* ni ile ya shilingi bilioni kwa ajili ya kuzima moto, kwenye miji ambayo iko kwenye *highway* magari yanagongana, mtu yuko hai gari limemminya, kuna vifaa vinahitajika vya kuvunja yale machuma, kukata, kuvuta ili kumtoa, watu wanakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *clips* tunazo, mtu alikufa pale Mbeya kwenye Mlima nadhani sijui ni Sekenke, watu wanamwangalia hawawezi kumwokoa. Kwa hiyo, kuna magari madogo labda yanahitajika na vifaa vidogo ambavyo halmashauri inaweza kutokana na eneo lake, basi iweze kufanya hivyo, siyo kuliondoa jukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jukumu la Serikali na mimi niseme hapa tunasaidiana, ndiyo maana ya ugatuzi, kwa sababu

Serikali itaendelea kuwekeza, hata leo ikiwekeza mara mbili ya hela mliyosema, bado mahitaji yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuseme kwa Dar es Salaam, kwa mfano hata kama mna magari matano, yametokea majanga mawili/matatu, lazima mtahitaji *manpower* zaidi na magari zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nimeitoa hoja hii ili Serikali iangalie namna ya kuboresha na kushirikiana, lakini halmashauri pia tunaona tuna wajibu wa kuwahudumia wananchi wetu na kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba Serikali ichukue hoja hii na iifanyie kazi pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na Wabunge na yale ambayo nilitoa mwanzo ili basi tuweze kuwahudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wabunge hawajasikia vizuri. Ili niweze kuwahoji, unatoa hoja tena. Kwa hiyo, hiyo sehemu ya mwisho hawajasikia.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, mawazo niliyoyaleta pamoja na mawazo yaliyoletwa na Wabunge, yale yote ambayo yana tija, ninaomba yachukuliwe na Serikali yafanyiwe kazi ili tuweze kuwahudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji kuhusu Hoja ya Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo kuhusu Halmashauri za Miji na Wilaya kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutatua tatizo

la upungufu wa magari ya Zimamoto pamoja na vifaa vinavyotumika kuzima moto na uokoaji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja Binafsi ya Mhe. Priscus J. Tarimo kuhusu Halmashauri za Miji na Wilaya Kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Kutatua Tatizo la Upungufu wa Magari ya Zimamoto pamoja na Vifaa Vinavyotumika Kuzima Moto na Uokoaji ilikubaliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote mmeafiki. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ninacheka kwa sababu sikujua huu ndiyo utakuwa mwisho wa hii hoja kwa namna michango mlivyoitoa humu ndani, lakini mmefanya vyema. Hoja imeungwa mkono kwa 100%, ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo kwa hoja yake ambayo ameileta hapa na ameweka maazimio aliyokuwa anayapendekeza kwa upande wa Bunge ili Bunge liweze kuazimia.

Sasa baada ya kuwahoji na ninyi kuitika ndiyo kwa 100%, mapendekezo aliyokuwa ameyaleta kama maazimo sasa yanakuwa ni Maazimio ya Bunge kuelekea Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nanyi ninawapongeza kwa pamoja kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge na kupitisha hoja yake hii ambayo sasa inakuwa ni Hoja ya Bunge na inakuwa Bunge limetoa maelekezo hayo kwa Serikali kama Maazimio. *(Makofi)*

Kwa hiyo, upande wa Serikali alipata nafasi ya kuchangia Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, lakini alishawahi kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa hiyo, ametoa mchango, lakini kwa ujumla wake kwa utaratibu ule wa kawaida, Bunge

likishaazimia basi Serikali inayachukua na kwenda kuyafanyia kazi kwa utaratibu ule wa kawaida.

Kwa hiyo, Serikali tunawatakia kila la kheri kwenda kuyafanyia kazi yale ambayo Bunge limeamua siku ya leo kupitia hoja ya Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo la wageni ambao wameingia baada ya tangazo la awali.

Kwanza, tunao wageni wenu Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 70 wa Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ambao ni viongozi na Wajumbe wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) kutoka Mkoa wa Katavi wakiongozwa na Ndugu Edna Buzima ambaye ni Katibu wa UWT Mkoa wa Katavi, karibuni sana, karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 72 wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Sekondari King'ori ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 90 wa Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle ambao ni Umoja wa Kikristo wa Wanafunzi Tanzania (UKWATA) kutoka Mkoa wa Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wapo wanafunzi 67 na walimu saba wa Shule ya Sekondari ya Kiadventista kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulio nao.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja hapa ambalo tangazo hili linatoka kwangu, tarehe 4 Juni, 2024 wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini aliuliza Swali Namba 518 kuhusu Serikali kuwalipa walimu wastaafu mafao yao. Katika maswali yake ya nyongeza aliuliza kuhusu uwepo wa changamoto kwa waajiri

kutopeleka michango ya watumishi katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiwepo *PSSSF*.

Pia alieleza baadhi ya walimu ambao wamelipwa walitakiwa kuchangia wenyewe mifuko hiyo badala ya mwajiri. *(Makofi)*

Baada ya kipindi cha maswali, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko aliomba Mwongozo kuhusiana na changamoto ya wastaafu kutakiwa kujilipia malimbikizo ya madeni ambayo mwajiri hajapeleka ili waweze kupewa mafao yao kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge.

Pia nilielekeza samahani, pia alieleza kuwa suala hili limekuwa likizungumzwa sana Bungeni kwenye michango mbalimbali wakati wa bajeti kwa miaka mingi mfululizo.

Waheshimiwa Wabunge, niliwapa nafasi upande wa Serikali na kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, alisema wanalichukua suala hili ili kwenda kulifanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kufuatilia mazungumzo ya Wabunge na Serikali, nilisema ninalielekeza suala hili kwa Kamati husika ili waweze kulifuatilia kwa ukamilifu ambapo Serikali itapata nafasi ya kupeleka taarifa zote muhimu, lakini sikuitaja Kamati hiyo inayohusika.

Hivyo basi, sasa ninalielekeza suala hili rasmi kushughulikiwa na Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii na itatuletea taarifa juu ya jambo hili wakati wa Mkutano ujao wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hilo ndiyo tangazo letu la mwisho na baada ya kusema hayo ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 6.03 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 7 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*